# UFUPISHO WENYE FAIDA KWA MWANAFUNZI MPYA

ABUU ADNAAN
HUSSEIN BIN AHMAD AL-MASQARY

بسم الله الرحمن الرحيم

# DAARUL HADITH

# MASJID SHEIKH ALBANY

## DAR-ES-SALAAM TANZANIA.

QUR'AN NA SUNNA,
KWA
UFAHAMU WA
WEMA WALIOTANGULIA.

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Hakika sifa njema zinamstahiki Allah, tunamuhimidi yeye na tunamtaka msaada na tunamtaka msamaha na tunajikinga kwa Allah kutokana na shari za nafsi zetu na kutokana na ubaya wa matendo yetu, mwenye kuongozwa na Allah hakuna wa kumpoteza na mwenye kupotezwa na Allah hakuna wa kumuongoza, na ninashuhudia kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake hana mshirika na ninashuhudia kuwa Muhammad ﷺ ni mja wake na mtume wake.

Hakika maneno bora ni maneno ya Allah, na muongozo ulio bora ni muongozo wa mtume Muhammad ﷺ Na mambo yenye shari ni yale yenye kuzushwa, na kila chenye kuzushwa ni bidaa na kila bidaa ni upotevu na kila upotevu ni motoni,

**قال الله تعالى {يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ} [آل عمران: 102]**

Amesema Allah, {**Enyi wale mlio amini! mcheni Allah ukweli wa kumcha na wala msife isipokuwa mfe hali ya kuwa ni waislamu**}. [Al imraan 102]

**قال الله تعالى {يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا} [النساء: 1]**

Amesema Allah, {**Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutokana na nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na mcheni Allah ambaye kupitia kwake mnaombana nyinyi kwa nyinyi, na jihadharini msije mkawakata jamaa zenu. Hakika Allah ni Mwenye kuwaangalieni**}. [nisaa 1]

وقال الله تعالى {يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا * يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَنْ يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا} [الأحزاب: 70، 71]

Na amesema Allah {**Enyi wale mlio amini! Mcheni Allah na semeni maneno ya sawasawa * atakutengenezeeni matendo yenu na atakusameheni madhambi yenu, Na anaye mt'ii Allah na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa**} [ahzaab 70-71]

Ama baada ya utangulizi;

Hii ni risala fupi katika baadhi ya misingi ya Elimu ya kitabu na sunna, pindi nilipoona kuwa wanafunzi wa Daarul-hadiith iliyopo Dar-es-salaam Tanzania kuwa ni wenye kuhitajia misingi ya kielimu, na wanao mwelekeo mkubwa juu ya kutafuta elimu ya kitabu na sunna, nimependelea nifanye ufupisho huu kwa wale wanaoanza kwa kile ambacho huenda kitawanufaisha wao na wengineo.

Na kwa hakika ametuhimiza juu ya jambo hili, ndugu Sheikh mbora Abuu Amru Al-Hajuriy Allah amuhifadhi na mwanangu mkarimu Sheikh Adnaan Allah amuhifadhi na amuwafikishe, na ninatarajia kutoka kwa Allah iwe risala hii ni kwa ajili ya uso wake na aijalie risala hii kukubaliwa katika nyoyo za waja wake. Na sifa njema zote ni za Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote.

## MAELEKEZO KWA MWALIMU

1. Inatakikana kwa mwalimu wa kitabu hiki, Allah amuafikishe, amchukulie mwanafunzi kutoka katika kila mlango, na katika kila shairi na katika kila dhikr kile ambacho kitakua chepesi kwa mwanafunzi kukifahamu na kukihifadhi, mpaka usije ukafika mwisho wa risala hii isipokuwa wameshahifadhi mashairi na mutuni na adhkaar kwa wepesi.
2. Na inatakikana atilie umuhimu kurudia rudia na kuwa na subira juu ya mwanafunzi mpaka ahifadhi.
3. Na asimzidishie mwanafunzi isipokuwa kwa kiasi cha hifidhi yake na hima yake, na lilokuwa bora asizidishe juu ya ubeti mmoja na dhikr moja kwa siku.

MWENYE KUWAFIKISHA NI ALLAH.

# AQIIDA

1. PINDI UTAKAPO ULIZWA, NI NANI MOLA WAKO?

Basi sema, mola wangu ni Allah peke yake, na dalili ni kauli yake Allah mtukufu

قال الله تعالى {الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ} [الفاتحة 1]

{**Sifa zote njema ni za Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote**}. [Al faatiha 1]

2. UTAKAPO ULIZWA, NI NANI NABII WAKO ?

Basi sema, nabii wangu ni Muhammad ﷺ, na dalili ni kauli yake Allah mtukufu

قال الله تعالى {مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ} [فتح 29]

{**Muhammad ni Mtume wa Allah...**}[fath 29]

3. UTAKAPO ULIZWA, NI KIPI KITABU CHAKO?

Basi sema, kitabu changu ni Qur’an, na dalili ni kauli yake Allah mtukufu

قال الله تعالى {كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ مُبَارَكٌ لِيَدَّبَّرُوا آيَاتِهِ وَلِيَتَذَكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ } [ص 29]

{**Na hiki Kitabu tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya zake, na wawaidhike wenye akili**}.[Swaad 29]

4. UTAKAPO ULIZWA, NI IPI DINI YAKO?

Basi sema, dini yangu ni uislamu, na dalili ni kauli yake Allah

قال الله تعالى {إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ}[آل عمران: 19]

{**Hakika Dini ya haki mbele ya Allah ni Uislamu**} [imran 19]

5. UTAKAPO ULIZWA, NI IPI AQIIDA YAKO ?

Basi sema, aqiida yangu ni, SUNNI SALAFIY, na salaf ni Muhammad ﷺ na Maswahaba zake ﷺ .

6. UTAKAPO ULIZWA NINI MAANA YA SUNNI SALAFIY?

Basi sema, SUNNI ni katika ahlu sunna wal-jamaa ambao wanahukumu kwa kitabu na sunna, na SALAFIY maana yake ni; naifahamu Qur'an na sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia katika umma huu(maswahaba).

7. UTAKAPO ULIZWA NI AKINA NANI WEMA WALIOTANGULIA?

Sema, ni Mtume wa Allah ﷺ na maswahaba رضي الله عنهم na wanaofuata baada yao.

8. NI NANI KIIGIZO CHAKO?

JIBU; ni Mtume wa Allah ﷺ amesema Allah,

**قال الله تعالى {لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَنْ كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا} [الأحزاب: 21]**

{**Hakika nyinyi mnacho kiigizo chema kwa Mtume wa Allah kwa anaye mtaraji Allah na Siku ya Mwisho, na akamtaja Allah sana**}.

9. NI NANI MUASISI WA AHLU SUNNA WAL-JAMAA NA KIONGOZI WAO?

JIBU, ni Mtume wa Allah ﷺ

10. NI NANI MUASISI WA KIKUNDI CHA IKH-WAAN MUSLIMIINA NA KIONGOZI WAO ?

JIBU, ni Hasani Al-banna, naye ni sufi mtu wa bidaa, nao wapo katika upotevu(masufi).

11. NI NANI MUASISI WA KIKUNDI CHA TABLIIGHI NA KIONGOZI WAO ?

JIBU, ni Muhammad bin Idrissa, nae ni sufi mtu wa bidaa, nao wapo katika upotevu(masufi).

12. NI NANI MUASISI WA MARAFIDHWA(MASHIA) NA KIONGOZI WAO ?

JIBU, ni Abdillah bin Sabaa myahudi.

13. NI IPI MAANA YA LAA ILAHA ILLA LLAH?

JIBU, maana yake ni, hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah pekee.

14. NI ZIPI NGUZO ZA LAA ILAHA ILLA LLAH?

JIBU, ni kukanusha na kuthibitisha.
Kukanusha ni kauli yake **Laa Ilaha**, na kuthibitisha ni kauli yake **Illa Llah**.

15. NI ZIPI SHARTI ZA LAA ILAHA ILLA LLAH ?

JIBU,
1]Elimu yenye kupingana na ujinga, Amesema Allah mtukufu,
**{فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنْبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مُتَقَلَّبَكُمْ وَمَثْوَاكُمْ} [محمد: 19]**

{**Basi jua ya kwamba, hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki ila Allah, na omba msamaha kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Allah anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa**}.[Muhammad 19]

2] Yaqiin yenye kupingana na shaka, amesema Allah mtukufu,
**{ذَلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِلْمُتَّقِينَ} [البقرة: 2]**
{**Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uwongofu kwa wamchao Allah**} [Al-baqara 2]
Na kutoka kwa Abuu Huraira ﷺ Amesema, "tulikuwa na Mtume ﷺ katika safari akasema, "**ninashuhudia kuwa hapana anaye stahiki kuabudiwa kwa haki ila Allah na mimi ni Mtume wa Allah hakutani na Allah mja yeyote kwa shahada hizo, hali yakuwa si mwenye kuwa na shaka isipokuwa ataingia peponi**". Ameipokea Muslim [27]

3] Ikhilas yenye kupingana na shiriki, Amesema Allah mtukufu,
**{إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ فَاعْبُدِ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ} [الزمر: 2]**
{**Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa Haki. Basi muabudu Allah hali ya kumtakasia Dini Yeye tu**}. [Zumar 2]

4] Ukweli wenye kupingana na uongo, Amesema Allah mtukufu,
**{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ} [التوبة: 119]**
**{Enyi wale mlio amini! Mcheni Allah, na kuweni pamoja na wakweli}.** [Tawba 119].

5] Mapenzi yenye kupingana na kuchukia, amesema Allah mtukufu,
**{قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ} [آل عمران: 31]**
{**Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Allah basi nifuateni mimi, Allah atakupendeni na atakusameheni madhambi yenu. Na Allah ni Mwenye kusamehe madhambi na Mwenye kurehemu}**. [Imran 31]

6] Kunyenyekea kwenye kupingana na kuacha, Amesema Allah mtukufu,
**{مَنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ وَمَنْ تَوَلَّى فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا} [النساء: 80]**
{**Mwenye kumt'ii Mtume basi ndio amemt'ii Allah. Na anaye kengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao**} [nisaa 80]

7] Kukubali kwenye kupingana na kurudisha, Amesema Allah mtukufu,
**{وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ} [الحشر: 7]**
{**Na alichokupeni Mtume basi kichukueni, na alicho kukatazeni basi jiepusheni nacho. Na mcheni Allah, Hakika Allah ni Mkali wa kuadhibu**}. [Hashir 7]

8] Kukufuru kila kisicho kuwa Allah, Amesema Allah mtukufu,
**{فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِنْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَى} [البقرة: 256]**

{**Basi yeyote mwenye kumkufuru twaghuti(yeyote anaye abudiwa asiyekuwa Allah) na akamuamini Allah bila shaka atakua amekamata kamba madhubuti**} [Baqara 256]

علـم يقين وإخلاص وصدقـك مع        محبــة وانـقيــاد والقبــول لـــــها
وزيـد ثامنـها الكفــران منــك بمــا        سوى الإلـه من المعبـود قد ألـها

Sharti za LAA ILAHA ILLA LLAH zimekusanywa katika ubeti huu,

**Elimu**, **yakini** na **ikhlas** na **kusadikisha** pamoja na **kupenda** na **kunyekea** na **kuikubali** na imezidishwa sharti ya nane **kukufuru vinavyo abudiwa kinyume na Allah**.

16 NI NINI MAANA YA MUHAMMAD MTUME WA ALLAH?

JIBU; yeye ni Mtume wa Allah kwa watu wote katika majini na wanadamu, Amesema Allah mtukufu,

{وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ} [سبأ: 28]

{**Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiriaji na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui**}. [Sabai 28]

17 NI LIPI LENYE KUHUKUMIWA NA SHAHADA YA KUWA MUHAMMAD NI MTUME WA ALLAH?

JIBU; maana yake, hapana anae fuatwa kwa haki isipokuwa Mtume wa Allah, na mwingineo asiye kuwa Mtume wa Allah ikiwa atafuatwa bila dalili basi ni batili, nae ni mtume wa Allah kwa watu wote, miongoni mwa majini na wanadamu. Amesema Allah mtukufu,

{وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ} [سبأ: 28]

{**Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiriaji na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui}**. [sabai 28]

Alipewa utume kwa surat Al-Muddathir(aya 5 za mwanzo) na akapewa unabii kwa surat Iqraa [aya 5 za mwanzo].

18 NI LIPI LENYE KUHUKUMIWA NA SHAHADA HII?

JIBU, ni kumtii mtume katika yale aliyoamrisha na kumusadikisha kwa yale aliyoyatolea habari na kujiepusha na yale aliyo yakataza na akayakemea, na tusimwabudu Allah isipokuwa kwa kile alicho kifanya kuwa ni sheria.

19 NI ZIPI DARAJA ZA DINI ?

JIBU, daraja za dini ni tatu, Uislamu na Imani na Ihsani. na dalili ni hadithi ya Umar bin Khatwaab ﵁ katika sahihi Muslim na ndani ya hadithi amesema, kuwa Jibril عليه السلام alimuuliza Mtume wa Allah ﷺ kuhusu Uislamu na Imani na Ihsani Alisema Jibril عليه السلام "nipe habari kuhusu Ihsani" akasema, "**ni kumwabudu Allah kana kwamba unamuona, ikiwa wewe humuoni, hakika yeye anakuona**".

20 UTAKAPO ULIZWA UISLAMU NI NINI?

JIBU; ni kujisalimisha kwa Allah kwa kumpwekesha yeye katika Ibada na kunyenyekea kwake kwa kumtii na kujivua kutokana na ushirikina na watu wake. Amesema Allah mtukufu,

**{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ} [آل عمران: 102]**

{**Enyi wale mlio amini! mcheni Allah ukweli wa kumcha na wala msife isipokuwa mfe hali ya kuwa ni waislamu**}.[imran 102]

21 NI ZIPI DALILI JUU YA UISLAMU ?

JIBU; Amesema Allah mtukufu,

**{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ} [آل عمران: 102]**

{**Enyi wale mlio amini! mcheni Allah ukweli wa kumcha na wala msife isipokuwa mfe hali ya kuwa ni waislamu**}. [Imran 102]

Amesema Allah mtukufu,

**{فَإِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ فَلَهُ أَسْلِمُوا وَبَشِّرِ الْمُخْبِتِينَ} [الحج: 34]**

{**Basi mwabudiwa wenu ni mwabudiwa Mmoja tu, basi jisalimisheni kwake tu na wabashirie wanyenyekevu**}.[Hajj 34]

Amesema Allah mtukufu

**{وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ} [آل عمران: 85]**

{**Na anaye tafuta dini isiyo kuwa ya Uislamu, haitokubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa miongoni mwa wenye khasara**}. [Imran 85]

**{الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا فَمَنِ اضْطُرَّ فِي مَخْمَصَةٍ غَيْرَ مُتَجَانِفٍ لِإِثْمٍ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ} [المائدة: 3]**

{**Leo hii nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekutimizieni juu yenu neema yangu, na nimeridhia UISLAMU uwe ndiyo Dini yenu. Na mwenye kulazimika kwasababu ya njaa akala(katika vile vilivyo haramishwa) chenye kumtosheleza kidharura(ili asife na njaa) bila ya kukusudia maasi, basi hakika Allah ni Msamehevu na Mwenye kurehemu**}.[Maida 3]

22 NI NGAPI NGUZO ZA UISLAMU?

JIBU; nguzo za uislamu ni tano,

1- Shahada ya kuwa hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na hakika Muhammad ﷺ ni mtume wa Allah.
2- Kusimamisha swala.
3- Kutoa zaka.

Amesema Allah mtukufu,

**{وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ وَذَلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ} [البينة: 5]**

{**Nao hawakuamrishwa kitu, isipokuwa wamuabudu Allah kwa kumtakasia dini, hali ya kuwa ni wenye kuelekea kwa Allah na wenye kupuuzia asiye kuwa Allah, na wasimamishe Swala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini madhubuti**}. [Bayyina-5]

4- Funga ya Ramadhani. Amesema Allah mtukufu,

**{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ} [البقرة: 183]**

{**Enyi wale mlio amini! Imefaradhishwa kwenu Saumu, kama ilivyo faradhishwa kwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kumcha Allah**} [Baqarah 183].

5- Hijja kwa mwenye kuweza njia. Amesema Allah mtukufu,

**{وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ} [آل عمران: 97]**

{**Ni haki ya Allah juu ya watu kuhiji nyumba hiyo(makka) kwa mwenye kuweza kwenda, Na atakaye kufuru basi Allah si mhitaji kwa walimwengu**}[imran 97]

Kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنه kutoka kwa mtume ﷺ Amesema, "**umejengwa uislamu juu ya nguzo tano, juu ya kumpwekesha Allah na kusimamisha Swala na kutoa Zaka na kufunga Ramadhani na kuhiji**". Ameipokea Muslim

Na kutoka kwa Abuu Huraira رضي الله عنه kutoka kwa mtume ﷺ Amesema, "**nimeamrishwa kupigana na watu mpaka washuhudie ya kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na waniamini mimi na kile nilicho kuja nacho, Basi wakifanya hivyo watakuwa wamezuia kutokana na mimi, damu zao na mali zao isipokuwa kwa haki ya uislamu, na hesebu yao ni kwa Allah**". Ameipokea muslim[1\52]

23 IMANI NI NINI?

JIBU, ni kutamka kwa ulimi, na kuitakidi kwa moyo, na kufanya vitendo kwa viungo, Inazidi kwa twa'a(kutii) na elimu, na inapungua kwa maasi na ujinga.

Amesema Allah mtukufu,

**{وَيَزْدَادَ الَّذِينَ آمَنُوا إِيمَانًا} [المدثر: 31]**

{**ili wazidi Imani wale walio amini**} [mudathir 31]

Kutoka kwa Abuu Said رضي الله عنه amesema, nilimsikia mtume ﷺ akisema, "**yeyote mwenye kuona munkari miongoni mwenu basi na aubadilishe kwa mkono wake, ikiwa hakuweza basi kwa ulimi wake, na ikiwa hakuweza basi kwa moyo wake, na huo ni udhaifu wa Imani**". Ameipokea Bukhari na Muslim.

24 NI ZIPI NGUZO ZA IMANI?
JIBU, nguzo za Imani ni sita. Na dalili ni hadithi ya Umar Ibn Khatwab ﵁ katika sahihi Muslim, Hakika ya mtume ﷺ aliulizwa na Jibril kuhusu Imani akasema, "**ni kumuamini Allah na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na kuamini Qadar kheri yake na shari yake"** akasema[Jibril] "umesema kweli"... na hadithi hii kaipokea pia Bukhari na Muslim kutoka kwa Abuu Huraira ﵁ .

25 IHSANI NI NINI ?
JIBU, ni kumwabudu Allah kana kwamba unamuona, ikiwa wewe humuoni hakika yeye anakuona. Kama ilivyo kuja katika hadithi ya Umar ﵁ ameipokea Muslim .

Amesema Allah mtukufu,
**{وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي أَنْفُسِكُمْ فَاحْذَرُوهُ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ} [البقرة: 235]**
{**Na jueni kwamba, hakika Allah anajua yaliyomo katika nafsi zenu. Basi tahadharini naye. Na jueni kwamba hakika Allah ni Mwenye kusamehe na Mpole**}. [Baqara 235]
Na amesema Allah mtukufu
**{يَعْلَمُ خَائِنَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفِي الصُّدُورُ} [غافر: 19]**
{**Anajua(Allah) khiyana ya macho, na yanayo fichwa na vifua**} [Ghaafir 19]

26 NI NINI MAANA YA IBADA ?
JIBU, Ibada ni jina linalokusanya kila anacho kipenda Allah na kukiridhia, katika vitendo na kauli za dhahiri na zilizo fichikana.
Amesema Allah mtukufu,
**{إِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنْكُمْ وَلَا يَرْضَى لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ وَإِنْ تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ } [الزمر: 7]**
{**Mkikufuru basi Allah si mwenye haja nanyi, lakini hafurahii kufuru kwa waja wake. Na mkishukuru ataliridhia hilo kwenu**} [Zumar 7]

27 TAUHIDI NI NINI ?
JIBU, ni kumpwekesha Allah katika Ibada.
Amesema Allah mtukufu,
**{وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا} [النساء: 36]**
{**Na muabuduni Allah, na wala msimshirikishe yeye na chochote**}[Nisaa 36]

Na amesema Allah mtukufu,

**{وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ فَمِنْهُمْ مَنْ هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَنْ حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ} [النحل: 36]**

{**Na kwa hakika katika kila umma tuliutumia Mtume, ya kwamba Muabuduni Allah, na muepukeni twaghuti, Basi miongoni mwao wapo alio waongoa Allah. Na kati yao wapo ambao uliowathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanao kanusha**}. [An-Nahli 36]

28 TAUHIDI INAGAWANYIKA VIGAWANYO VINGAPI?

JIBU, Tauhidi inagawanyika vigawanyo vitatu,

1: Tauhid Rububiyya, na maana yake ni kumpwekesha Allah kwa vitendo vyake.

2: Tauhid al-uluhiyya, na maana yake ni kumpwekesha Allah kwa vitendo vya waja wake.

3: Tauhid al-as`maa wa swifaat, nayo ni; tumsifu Allah kwa alichojisifu nacho yeye mwenyewe, au alichosifiwa na mtume wake, na tukanushe kwake kile alichojikanushia nafsi yake, na akakikanusha kitu hicho mtume wake. Amesema Allah mtukufu,

**{وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَى فَادْعُوهُ بِهَا وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ} [الأعراف: 180]**

{**Na Allah ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwayo. Na waacheni wale wanao pindisha katika majina yake. Hao watakuja lipwa waliyo kuwa wakiyatenda**}. [A'araf 180]

Amesema Allah mtukufu,

**{لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ} [الشورى: 11]**

{**Hapana chochote mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona**} [Shuraa 11]

29 NI IPI HAKI YA ALLAH JUU YA WAJA, NA NI IPI HAKI YA WAJA JUU YA ALLAH?

JIBU, haki ya Allah juu ya waja ni wamuabudu yeye wala wasimshirikishe na chochote na haki ya waja juu ya Allah ni, hato muadhibu yule ambaye hamshirikishi yeye na chochote. Na dalili ni hadithi ya Muadh ﵁ Amesema, amesema mtume ﷺ , "ewe

Muadh hivi unajua ni ipi haki ya Allah juu ya waja na haki ya waja juu ya Allah? akasema(Muadh), “Allah na mtume wake ni wajuzi zaidi”. Akasema, “**haki ya Allah juu ya waja ni wamwabudu yeye wala wasimshirikishe na chochote na haki ya waja juu ya Allah ni hamuadhibu yule asiye mshirikisha na chochote**” Ameipokea Bukhari na Muslim na hii ni lafdhi ya Bukhari.

30 TAJA WEMA MKUBWA ZAIDI NA UOVU MKUBWA ZAIDI?

JIBU, wema mkubwa zaidi ni kumpwekesha Allah mwenye nguvu aliyetukuka katika ibada, na dalili kutoka kwa Uthmaan رضي الله عنه, Amesema, amesema mtume wa Allah صلى الله عليه وسلم “**yeyote mwenye kufa hali ya kuwa anajua kuwa hapana mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki ila Allah ataingia peponi**”. Ameipokea Muslim.

Na uovu mkubwa zaidi ni, kumshirikisha Allah mwenye nguvu aliyetukuka. Amesema Allah mtukufu,

**{إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَى إِثْمًا عَظِيمًا} [النساء: 48]**

{**Hakika Allah hamsamehe mwenye kumshirikisha, na husamehe yaliyo chini ya hilo(shirki) kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Allah basi hakika amezua dhambi iliyo kubwa**}. [Nisaa 48]

31 SHIRKI NI NINI?

JIBU, shirki ni kumwabudia asiye kuwa Allah mwenye nguvu aliye tukuka. Na kila kinacho kuwa ibada kwa ajili ya Allah kukigeuza kwa asiye kuwa Allah ni shirki. Amesema Allah mtukufu,

**{وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا} [النساء: 36]**

{**Muabuduni Allah wala msimshirikishe na chochote**}[nisaa 36]

32 NI IPI HAKI KATIKA MAJINA YA ALLAH NA SIFA ZAKE ?

JIBU, haki katika majina ya Allah na sifa zake ni tuyathibitishe kama yalivyo kuja hatuyakanushi wala hatuyapingi wala hatumfananishi Allah Na viumbe Wake.

33 NI IPI KAULI YA WATU WA HAKI KATIKA QUR’AN?

JIBU, wanasema, ni maneno ya Allah si kiumbe, kwake yameanza na kwake yatarejea.

34 NI AKINA NANI AMBAO WANAPINGA MAJINA YA ALLAH NA SIFA ZAKE?

JIBU, ni MAJAHAMIYA (wafuasi wa Jaham bin Swafwaan).

35 NI AKINA NANI AMBAO WANAPINGA SIFA ZA ALLAH?

JIBU, ni MUU’TAZILA (wafuasi wa Waswil bin Atwaa).

36 NI AKINA NANI AMBAO WAMEPINGA SIFA ISIPOKUWA SIFA SABA TU?

JIBU, ni AL’ASHAAIRA.

37 NI AKINA NANI AMBAO WANAPINGA HODHI NA MIZANI NA SWIRAATWI?

JIBU, ni MUU’TAZILA kwa kuhukumia akili zao. Na dalili juu ya kuthibitisha hodhi na mizani na swiratwi ni nyingi.

38 NI IPI KAULI YA WATU WA SUNNA KATIKA PEPO NA MOTO ?

JIBU, wanasema, hakika ya pepo na moto vipo, vimeumbwa na haviishi wala haviharibiki.

39 NI AKINA NANI AMBAO WANATUKANA MASWAHABA WA MTUME ﷺ ?

JIBU, ni MARAFIDHWA(MASHIA).

40 NI AKINA NANI AMBAO WANATOKA JUU YA KIONGOZI NA WANAWAKUFURISHA WAISLAMU?

JIBU: ni MAKHAWARIJ, na kila mtu wa bidaa ni Khawarij amesema mtume ﷺ “**yeyote mwenye kuona kwa kiongozi wake kitu anakichukia basi asubiri, hakika mwenye kufarikiana na jamaa kiasi cha shibri moja, akafa basi kufa kwake ni kwa kijahiliya(kijinga)**” Ameipokea Bukhari na Muslim [1849] kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه .

41 NI AKINA NANI AMBAO WAMEPINGA QADARI?

JIBU: ni QADARIYA (wafuasi wa Ma’abadi Al-juhaniy).

42 NI ZIPI DARAJA ZA QADARI?

JIBU: ni nne: elimu, uandishi, matashi na uumbaji.

43 JE, NDANI YA KABURI KUNA ADHABU?

JIBU: ndiyo, amesema mtume ﷺ, “**Adhabu ya kaburi ni haki**” Ameipokea Bukhari.

44 NINI ANAULIZWA MJA KATIKA KABURI LAKE ?

JIBU: anaulizwa, ni nani mola wako? na ni ipi dini yako? na ni nani nabii wako?.

45 NA NINI ANAULIZWA SIKU YA KIAMA?

JIBU: anaulizwa kuhusu Ikhlaas, na kumfuata mtume ﷺ na kuhusu damu. Amesema Allah,

{وَقِيلَ لَهُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ} [الشعراء: 92]

**{Na wataambiwa: Wako wapi mlio kuwa mkiwaabudu?}** [shuaraa 92]

Na amesema Allah mtukufu,

{وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ مَاذَا أَجَبْتُمُ الْمُرْسَلِينَ } [القصص: 65]

{**Na siku atakapo waita na akasema: Mliwajibu nini Mitume?**} [qasas 65]

Na kutoka kwa Ibn Masuud رضي الله عنه Amesema, amesema mtume ﷺ, "**kitu cha mwazo kitakacho hukumiwa baina ya watu siku ya kiyama ni katika damu**". Ameipokea Bukhari na Muslim.

46 JE INAJUZU KUWAKUFURISHA WAISLAMU NA KUTOKA JUU YAO?

JIBU: haijuzu, Amesema mtume ﷺ, "**atakapo mkufurisha mtu ndugu yake(muislam) kwa hakika atakuwa amerejea na ukafiri huo mmoja wao**". Ameipokea Bukhari na Muslim kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنه [60]

47 TAJA NASABA YA MTUME ﷺ?

JIBU: ni Muhammad bin Abdillah bin Abdi l'mutwalib bin Haashim bin Abdil manaa'fi bin Qusway bin Kilaab bin Murra bin kaa'bi bin Luay.

48 KWA KITU GANI KAFADHILISHWA MTUME ﷺ?

JIBU: Allah kamfadhilisha kwa mambo mengi, miongoni mwayo ni; kuwa yeye ni bwana wa watu na amepewa uombezi mkubwa. Amesema mtume ﷺ, "**Nimefadhilishwa juu ya manabii kwa mambo sita; nimepewa maneno ya ujumla, na nimenusuriwa kwa kuogopwa kwa mwendo wa mwezi mmoja, na zimehalalishwa kwangu mimi ngawira, na imejaliwa kwangu mimi ardhi kuwa ni twahara na sehemu ya kuswalia, na**

**nimetumwa kwa viumbe wote, na wamekhitimishwa kwangu manabii**”. Ameipokea Muslim kutoka kwa Abuu Huraira ﷺ .

49 NI NANI MTUME WA MWANZO KWA WATU WA ARDHINI?

JIBU: wa mwanzo wao ni Nuhu ﷺ, na wa mwisho wao ni Muhammad ﷺ. na dalili ni kauli ya Allah mtukufu,

**{إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ} [النساء: 163]**

{**Hakika Sisi tumekuletea wahyi wewe kama tulivyo wapelekea wahyi Nuhu na Manabii walio kuwa baada yake**}. [Nisaa 163]

50 INAJUZU KUFARIKIANA KATIKA DINI?

JIBU: Haijuzu, nako ni kujifananisha na makafiri. Amesema Allah mtukufu,

**{وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا} [آل عمران: 103]**

{**Na shikamaneni kwa Kamba ya Allah nyote pamoja, wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu, pindi mlivyo kuwa nyinyi kwa nyinyi maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema yake mkawa ndugu**}. [imran 103]

51 NI IPI HUKUMU YA ANAE FUATA MIFARAKANO NA MAKUNDI YA KIISLAMU?

JIBU: ni Mzushi, Kwa sababu kufanya umakundi ni uzushi katika dini na kuabudia bila ya dalili. Amesema mtume ﷺ “**Hakika ya wana wa Isra’ili waligawanyika makundi sabini na mbili, na utagawanyika umma wangu makundi sabini na tatu, yote hayo ni motoni isipokuwa moja**, wakasema: ni lipi hilo ewe mtume wa Allah? Akasema, “**ni lile ambalo mimi niko juu yake leo na maswahaba wangu**”. Ameipokea Tirimidh [2641] nayo ni hadithi iliyothibiti.

52 JE INAFAA KWA MUISLAM KUFANYA MAKABURI KUWA MISIKITI?

JIBU: Haifai kwa kauli ya mtume ﷺ "**msiswali kwa kuyaelekea makaburi wala msikae juu yake**". Ameipokea Muslim

53 JE INAFAA KUOMBA MVUA KWA KUTUMIA NYOTA?

JIBU: Haifai. amesema Allah mtukufu,

**{وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَنَّكُمْ تُكَذِّبُونَ} [الواقعة: 82]**

{**Na badala ya kushukuru kwa riziki yenu mnafanya kuwa mnakadhibisha?**} [waaqiya 82]

54 JE INAFAA KWENDA KWA WACHAWI NA MAKUHANI NA WAPIGA RAMLI?

JIBU: Haifai, kwa hadithi ya Swafiya رضي الله عنها, kutoka kwa baadhi ya wake za mtume ﷺ kutoka kwa mtume ﷺ Amesema, " **Yeyote mwenye kumwendea mpiga ramli akamuuliza chochote, haitokubaliwa swala yake siku arobaini**". Ameipokea Muslim [2230]

Na mpiga ramli ni jumla ya aina za makuhani. Amesema Khatwib na wengineo: Mpiga ramli ni yule ambaye anajilazimisha kufahamu sehemu kiliko kitu kilicho ibiwa au sehemu kilipo kitu kilicho potea na mfano wa hivyo.

55 JE INAFAA KUFANYA TA'TWAYYUR[kuona nuksi]?

JIBU: Haifai, na ni katika matendo ya watu wa jaahiliya. Amesema Allah mtukufu,

**{قَالَ طَائِرُكُمْ عِنْدَ اللَّهِ} [النمل: 47]**

{**Akasema mkosi wenu uko kwa Allah**}. [namli 47]

56 NI IPI HUKUMU YA MWENYE KUMKUFURU MTUME MIONGONI MWA MITUME?

JIBU: Hukumu yake ni kafiri. Amesema Allah mtukufu,

**{إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُونَ نُؤْمِنُ بِبَعْضٍ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ وَيُرِيدُونَ أَنْ يَتَّخِذُوا بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا * أُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ حَقًّا وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُهِينًا} [النساء: 150، 151]**

{**Hakika wale wanao mkufuru Allah na Mitume wake, na wanataka kufarikisha baina ya Allah na Mitume wake, kwa kusema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakufuru. Na wanataka kufanya baina ya hilo kuwa ndio njia. Hao ndio makafiri kweli. Na tumewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha**}. [Nisaa 150-151]

57 UTAKAPO ULIZWA NI YAPI MAZURI YA UISLAMU UPANDE WA MUISLAMU?

BASI SEMA: Miongoni mwa mazuri ya uislamu upande wa muislamu ni kuwatii wazazi wawili na ujirani mzuri na kutoa salamu na kuunganisha udugu na ukweli pamoja na watu katika miamala nao.

58 NI YAPI MAZURI YA UISLAMU UPANDE WA MAKAFIRI?

JIBU: Ukweli pamoja nao na kutekeleza Ahadi na uharamu wa kukhalifu makubaliano na uharamu wa kumuua kafiri mwenye ahadi(muda wa kuishi kwa amani) na kuwaombea uongofu.

59 NI ZIPI ALAMA ZA MNAFKI?

JIBU: Ni pindi anapo hadithia husema uongo, na anapo ahidi hukhalifu(hatekelezi) na akiaminiwa hufanya khiyana. kwa hadithi ya Abuu Huraira ﵁ katika sahihi mbili kutoka kwa mtume ﷺ.

60 TAJA DUA TATU ZENYE MANENO YA UJUMLA?

JIBU:

**«اللهُمَّ أَصْلِحْ لِي دِينِي الَّذِي هُوَ عِصْمَةُ أَمْرِي، وَأَصْلِحْ لِي دُنْيَايَ الَّتِي فِيهَا مَعَاشِي، وَأَصْلِحْ لِي آخِرَتِي الَّتِي فِيهَا مَعَادِي، وَاجْعَلِ الْحَيَاةَ زِيَادَةً لِي فِي كُلِّ خَيْرٍ، وَاجْعَلِ الْمَوْتَ رَاحَةً لِي مِنْ كُلِّ شَرٍّ»**

«**Ewe Allah nitengenezee dini yangu ambayo ni kinga au ulinzi wa jambo langu, na nitengenezee dunia yangu ambayo ndani yake kuna maisha yangu, na nitengenezee akhera yangu ambayo kuna marejeo yangu, na jalia uhai kuwa ni ziada**

**kwangu katika kila kheri, na jalia umauti kuwa raha kwangu kutokana na kila shari**». Ameipokea Muslim [2720]

«اللهُمَّ إني أسألك العفو العافية »

«**Ewe Allah hakika mimi nakuomba msamaha na afya**».

«اللهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عِلْمٍ لَا يَنْفَعُ، وَمِنْ قَلْبٍ لَا يَخْشَعُ، وَمِنْ نَفْسٍ لَا تَشْبَعُ، وَمِنْ دَعْوَةٍ لَا يُسْتَجَابُ لَهَا»

«**Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na elimu isiyo nufaisha, na kutokana na moyo usio ogopa, na kutokana na nafsi isiyo shiba, na kutokana na maombi(duaa) yasiyo itikiwa**» kutoka kwa Zaidi bin Arqam ﵁ . Ameipokea Muslimu [2722] na kutoka kwa Abuu Huraira ﵁ . Ameipokea Abuu Daudi [2/92].

61 NI NINI ANASEMA MTU PINDI ANAPO SILIMU?

JIBU: Anasema pindi anapokuwa muislamu,

«اللهُمَّ اغْفِرْ لِي، وَارْحَمْنِي، وَاهْدِنِي، وَعَافِنِي، وَارْزُقْنِي»

**«Ewe Allah nisamehe mimi na unirehemu na uniongoze na unipe afya na uniruzuku**».

Kutoka kwa Twariq bin Ash-yam ﵁ Amesema, alikuwa mtu akisilimu, mtume ﷺ anamfundisha swala kisha anamuamrisha aombe kwa maneno haya "**Ewe Allah ....**". Ameipokea Muslim [2697]

62 NI YAPI MASHARTI YA KUKUBALIWA KWA MATENDO?

JIBU: 1) Uislamu. Allah hakubali tendo lolote la kafiri.

2) Ikhlas. Amesema Allah mtukufu,

{وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ} [البينة: 5]

{**Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Allah kwa kumtakasia yeye Dini**} [Bayyinah 5]

3) Kumfuata mtume ﷺ kwa kauli ya mtume ﷺ "**mwenye kufanya tendo lolote hakuna juu yake amri yetu basi ni lenye kurudishwa**". Ameipokea Muslim kutoka kwa Aisha رضي الله عنها .

63 NI VIPI VITENGUZI VYA UISLAMU?

JIBU: Fahamu ya kuwa miongoni mwa vitenguzi vikubwa vya uislamu ni kumi;

1- Kufanya ushirikina katika ibada ya Allah peke yake hana mshirika, na dalili ni kauli yake Allah mtukufu,

**{ إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ} [النساء: 48]**

{**Hakika Allah hasamehe kushirikishwa, na husamehe(dhambi) iliyo chini ya hilo(shirki) kwa amtakaye**} [Nisaa 48]

2- Mwenye kujalia baina yake na baina ya Allah waunganishi, akawa anawaomba wao na anawataka wao uombezi kwa Allah, atakuwa amekufuru kwa makubaliano ya wachuoni.

3- Yule asiye wakufurisha washirikina au akawa na shaka juu ya kufru yao au akasahihisha nyenendo zao, atakuwa amekufuru kwa makubaliano ya wanachuoni.

4- Mwenye kuitakidi kuwa mwongozo usio wa mtume ﷺ ni mkamilifu zaidi kuliko mwongozo wake, basi mtu huyo ni kafiri.

5- Mwenye kuchukia chochote miongoni mwa vile alivyo kuja navyo mtume ﷺ na hata kama atakifanyia kazi, atakuwa amekufuru kwa makubaliano ya wanachuoni. Na dalili ni kauli yake Allah mtukufu,

**{ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ} [محمد: 9]**

{**Hivyo ni kwa sababu waliyachukia aliyo yateremsha Allah, basi akaviporomosha vitendo vyao**}. [Muhammad 9]

6- Mwenye kufanyia masikhara chochote katika dini ya Allah au malipo yake au adhabu yake, atakuwa amekufuru. Na dalili ni kauli yake Allah mtukufu

**{قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ * لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ} [التوبة: 65، 66]**

{**Sema: Je, Mlikuwa mkimfanyia maskhara Allah na Aya zake na Mtume wake? * Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu!**}[Tawba 65-66]

7- Uchawi, na mingoni mwa uchawi ni kufarakanisha na kuunganisha, basi mwenye kuufanya au akauridhia atakuwa amekufuru, na dalili ni kauli yake Allah mtukufu,

**{وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ} [البقرة: 102]**

{**Wala hao hawakuwa wanamfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni fitna(mtihani); basi usikufuru**}. [Baqara 102]

8- Kuwasaidia makafiri dhidi ya waislamu, na dalili ni kauli yake Allah mtukufu,

**{وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ} [المائدة: 51]**

{**Na mwenye kufanya urafiki nao(makafiri) miongoni mwenu, basi huyo ni katika wao. Hakika Allah hawaongoi watu wenye kudhulumu**}. [Maida 51]

9- Mwenye kuitakidi kuwa baadhi ya watu sio wajibu kwao kumfuata mtume ﷺ na kuwa inawezekana kwao kutoka katika sheria ya mtume, basi mtu huyu ni kafiri.

10- Kuipuuzia dini ya Allah, akawa mtu hajifundishi wala haifanyii kazi. Na dalili ni kauli yake Allah mtukufu,

**{وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنْتَقِمُونَ} [السجدة: 22]**

{**Na ni nani dhaalimu mkubwa zaidi kuliko yule anaye kumbushwa kwa aya za Mola wake Mlezi, kisha anazipuuza? Hakika Sisi ni wenye kuwaadhibu waovu**}. [Sajda 22]

64 NI YAPI MAMBO YA KIJAHILIYA(ZAMA KABLA YA UISLAMU) AMBAYO UMEJIPAMBANUA UISLAMU KWA KUYAKATAZA NA KUYATAHADHARISHA NA KUYABADILISHA?

JIBU: Ametaja Imam An-najidiy Allah amrehemu mambo miogoni mwayo ni,

Moja: Hakika wao walikuwa wakiabudia kwa kumshirikisha katika kumuomba Allah na ibada yake. Amesema Allah mtukufu,

**{وَيَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِنْدَ اللَّهِ} [يونس: 18]**

{**Wanaabudu kinyume na Allah vile visivyo wadhuru wala kuwanufaisha, na wanasema: Hawa ndio waombezi wetu kwa Allah**} [Yunus 18]

Mbili: hakika wao ni wenye kutofautiana katika dini yao. Amesema Allah mtukufu hali ya kuwa ni mwenye kukataza kutokana na kujifananisha nao kwa kauli yake,

**{وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَفَرَّقُوا وَاخْتَلَفُوا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ} [آل عمران: 105]**

{**Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kukhitalifiana baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi}**. [Imran 105]

Tatu: Kumkhalifu kiongozi na kutokumtii.

Na haya ndiyo matatu ambayo ameyakusanya mtume ﷺ katika yale aliyoyasema, "**Hakika ya Allah anaridhia kwenu nyinyi mambo matatu: msiabudu isipokuwa Allah wala msimshirikishe na chochote, na mshikamane na kamba ya Allah nyote wala msifarakiane, na mumnasihi yule ambaye Allah amemtawalishia jambo lenu"** haikutokea mianya katika dini ya watu na dunia yao, isipokuwa kwa sababu ya mianya katika mambo haya matatu au baadhi yake.

Nne: hakika ya dini yao imejengeka juu ya kuiga, kama alivyosema Allah mtukufu,

**{وَإِنَّا عَلَى آثَارِهِمْ مُقْتَدُونَ} [الزخرف: 23]**

{**Hakika sisi ni wenye kuiga nyayo zao**}. [Zukhruf 23]

Tano: Kughurika na wingi, na wanatolea hoja kwa wingi juu ya kusihi kitu.

**{وَقَالُوا نَحْنُ أَكْثَرُ أَمْوَالًا وَأَوْلَادًا وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِينَ} [سبأ: 35]**

{**Na wakasema: Sisi tuna mali nyingi zaidi na watoto, wala sisi hatutaadhibiwa}** [Sabai 35]

Sita: Kutolea hoja kwa walio tangulia, kama vile kauli yake Allah mtukufu,

**{قَالَ فَمَا بَالُ الْقُرُونِ الْأُولَى} [طه: 51]**
{**Nini hali ya karne za kwanza?**} [Twaha 51]

**{مَا سَمِعْنَا بِهَذَا فِي آبَائِنَا الْأَوَّلِينَ} [المؤمنون: 24]**
{**Hatukusikia haya kwa baba zetu wa zamani**}. [Muuminun 24]

Saba: Kustadili na watu waliopewa Ufalme na mali na cheo, Allah akalirudi hilo kwa kauli yake,
**{وَكَانُوا مِنْ قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ} [البقرة: 89]**
{**na wao walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri. Na pindi yalipo wajia yale waliyo kuwa wakiyajua waliyakufuru}**. [Baqara 89]

Nane: kutolea hoja juu ya ubatili wa kitu kuwa hawakukifuata isipokuwa watu madhaifu, kama vile kauli yake Allah,
**{قَالُوا أَنُؤْمِنُ لَكَ وَاتَّبَعَكَ الْأَرْذَلُونَ} [الشعراء: 111]**
{**Je! Tukuamini wewe, hali wanao kufuata ni watu wa chini(madhalili)?}** [Shuaraa 111]

Tisa: Kufuata wanachuoni waovu. imekuja katika kauli yake Allah akisema,
**{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ كَثِيرًا مِنَ الْأَحْبَارِ وَالرُّهْبَانِ لَيَأْكُلُونَ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ} [التوبة: 34]**
{**Enyi wale mlio amini! Hakika wengi miongoni mwa wanazuoni wa kiyahudi na miongoni mwa wafanya ibada wa manaswara, wanakula mali za watu kwa batili na wanazuilia Njia ya Allah**} [Tawba 34]

Kumi: Taasubb(Ung’ang’anizi) wa koo na nasaba. Kwa hakika amesema mtume ﷺ, “**mambo manne katika umma wangu ni katika mambo ya ujinga, hawayaachi mambo hayo, kujifakharisha na koo na kutukana nasaba….**” hadithi iko katika Muslim.

65 JE, WAUMINI WATAMUONA MOLA WAO?

JIBU: Ndiyo watamuona mola wao mara mbili;

1) Watamuona katika viwanja vya kiama, kinyume na makafiri Amesema Allah,

{كَلَّا إِنَّهُمْ عَنْ رَبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَمَحْجُوبُونَ} [المطففين: 15]

{**Hasha! Hakika hao siku hiyo kutokana na kumuona Mlezi wao ni wenye kuzuiliwa**}. [Mutaffifin 15]

Na amesema Allah mtukufu,

{وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَاضِرَةٌ * إِلَى رَبِّهَا نَاظِرَةٌ} [القيامة: 22، 23]

{**Nyuso siku hiyo ni zenye kung'ara * kwa mola wao mlezi ni zenye kumuangalia**} [Qiyama 22-23]

2) Na watamuona katika pepo. Amesema Allah mtukufu,

{لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَى وَزِيَادَةٌ وَلَا يَرْهَقُ وُجُوهَهُمْ قَتَرٌ وَلَا ذِلَّةٌ أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ } [يونس: 26]

{**Wanayo wale waliyofanya mema, pepo na ziada(kumuona Allah). Na wala vumbi halitawafunika nyuso zao, wala udhalili. Hao ndio watu wa Peponi. Humo watadumu milele**} [Yunus 26]

Na amesema Ibn Taymiyah Allah amrehemu,

والمؤمنـون يـرون حقـا ربهـم وإلى السمـاء بغيـر كيـف ينـزل

Maana ya ubeti, "Na waumini watamuona kwa haki mlezi wao na kuielekea mbingu ya dunia anateremka pasina namna.

66 NI IPI HUKUMU YA KUJIFUNDISHA ELIMU?

JIBU: Ni wajibu. Na Elimu ya wajibu kujifundisha ni; elimu ya kumjua Allah na mtume wake na Dini yake kwa dalili za kisheria. Amesema Allah mtukufu,

{فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنْبِكَ} [محمد: 19]

{**Basi jua ya kwamba hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na taka msamaha kwa dhambi zako**}. [Muhammad 19]

- Na elimu ambayo inayojuzu kujifundisha, Nayo ni kujifundisha elimu ya dunia na Udaktari na elimu nyinginezo za kidunia.

- Na elimu ambayo ni haramu kujifundisha: Nayo ni kujifundisha elimu ya uchawi, na ya watu wa bid'aa na batili na miongoni mwazo ni elimu ya Sayansi ya Qur'an.

67 NI VIPI VIGAWANYO VYA SHIRIKI?

JIBU: Shirki kubwa, na inakuwa katika Tauhidi ya ulezi au katika Tauhidi ya ibada. nayo ni yenye kumtoa mtu katika dini ya kiislamu.
Na Shirki ndogo, nayo inakuwa katika Tauhidi ya ulezi au katika Tauhidi ya ibada. nayo ni ile ambayo inakuwa kwa matamshi au kimatendo. Lakini haimtoi mtu katika dini ya kiislamu.

68 NI VIPI VIGAWANYO VYA TAWASSUL?

JIBU: 1. Tawassul inayofaa kisheria, nayo ina vigawanyo vitatu;
1- Kufanya tawassul kwa majina ya Allah na sifa zake.
2- Kufanya tawassul kwa matendo mema.
3- Kufanya tawassul kwa Dua ya mtu mwema.
2. Tawassul iliyo katazwa kisheria, nayo ni kufanya tawassul kwa mawalii na wafu(maiti) na majini na wegineo.

69 NI VIPI VIGAWANYO VYA DUA?

JIBU : 1) Dua ambayo ni Ibada, kama vile swala na hijja.
2) Dua ya maombi, nayo ni kumuomba Allah na kumtaka msaada na kumtaka kinga na kumtaka uokozi.

70 NI VIPI VIGAWANYO VYA TAWAKKUL?

JIBU: Tawakkul ni kuwa mkweli na Allah na kumtegemea katika kutafuta manufaa na kuzuia madhara. Ina vigawanyo viwili:
1) Kumtegemea Allah katika mambo ya kidunia tu.
2) Kumtegemea Allah katika mambo ya kidunia na kidini. na hii ni tawakkul bora zaidi.

71 NI VIPI VIGAWANYO VYA MAHABBA?

JIBU: 1) Mahabba ya kisheria ambayo ni Ibada.
2) Mahabba ya kishirikina, nayo ni kuwapenda washirika kama anavyopendwa Allah mtukufu.

3) Mahabba ambayo ni maasi, kama kuwapenda watu waovu na miziki na mapicha na mambo ya haramu.
4) Mahabba ya kimaumbile, kama vile mahabba ya kumpenda mzazi mtoto wake na mkewe.

72 NI VIPI VIGAWANYO VYA KHOFU?

JIBU: 1) Khofu ya kisheria, nayo ni Ibada. nayo ni kumuogopa Allah na moto wake na ghadhabu(hasira) zake na adhabu zake.

2) khofu ya kishirikina, nayo ni kuogopa washirika(miungu) na masanamu na vinginevyo.

3) Khofu ambayo ni maasi, kama vile kuwaogopa watu mpaka mtu anaingia katika maasi.

4) Khofu ya kimaumbile, nayo ni kama kumuogopa nyoka na kiza na vinginevyo.

73 NI VIPI VIGAWANYO VYA ISTI'GHAATHA(KUTAFUTA UOKOZI)?

JIBU: 1) Isti'ghaatha ya kisheria, nayo ni kutafuta uokozi kwa Allah kwa mapenzi na woga.

2) Isti'ghaatha ya kishirikina, nayo ni kutafuta uokozi kwa majini na mawalii kwa ajili ya kuzuia madhara au kutafuta manufaa. Hii haifai.

3) Isti'ghaatha inayojuzu, nayo ni kutaka uokozi kwa mtu aliye hai mwenye uwezo ambaye yuko eneo la tukio.

**{فَاسْتَغَاثَهُ الَّذِي مِنْ شِيعَتِهِ عَلَى الَّذِي مِنْ عَدُوِّهِ} [القصص: 15]**

{**Basi yule aliyekuwa katika watu wa musa, alimtaka msaada dhidi ya adui wake**}. [Qasas 15]

74 NI VIPI VIGAWANYO VYA RUQIYA?

JIBU: 1) Ruqiya ya kisheria, Nayo ni ile ambayo inakuwa kwa Qur’ani na Sunna na kwa lugha ya kiarabu.

2)Ruqiya iliyokatazwa, nayo ni ile ambayo inakuwa kwa hirizi na nyiradi za kishirikina na matamko yasiyo fahamika.

75 NI VIPI VIGAWANYO VYA UCHAWI?

JIBU: Uchawi ni ukafiri. Amesema Allah mtukufu,
**{وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ} [البقرة: 102]**
{**Na wala Suleiman hakukufuru, bali mashetani ndio walio kufuru, wanawafundisha watu uchawi**} [Baqara 102]

1) Uchawi wa kuunganisha, nao ni uchawi wa kupendezesha baina ya mtu na mtu.

2) Na uchawi wa kufarakanisha, nao ni uchawi wa kutengeneza chuki baina ya mtu na mtu.

76 NI VIPI VIGAWANYO VYA UOMBEZI?

JIBU: 1) Uombezi wenye kurudishwa: nao ni ule ambao umekanushwa na Qur’an, nao ni ule ambao unakuwa kwa ajili ya mshirikina au ukawa unatoka kwa mshirikina.

2) Uombezi wenye kukubaliwa, nao ni ule ambao unatoka kwa mtu mwenye kumpwekesha Allah au unakuwa kwa ajili ya mtu anaye mpwekesha Allah. Na uombezi huu una aina nyingi;

1- Uombezi mkubwa nao ni uombezi wake mtume ﷺ kuwaombea watu wa kisimamo, wahukumiwe baina yao, nacho ndiyo kisimamo chenye kusifiwa, na uombezi huu ni miongoni mwa mambo ya kipekee ya mtume wetu ﷺ juu ya wengineo katika mitume swala za Allah ziwe juu yao wote.

2- Uombezi wake mtume ﷺ kwa baba yake mdogo Abuu Twaalib ili apunguziwe adhabu.

3- Uombezi wake mtume ﷺ kwa watu wa peponi ili wapewe idhini ya kuingia peponi, na uombezi huu ni wa mtume wetu Muhammad ﷺ pekee.

4- Uombezi wake mtume ﷺ kwa kikundi cha watu kuingia peponi bila ya hesabu.

5- Uombezi wake mtume ﷺ kuwaombea watu wa madhambi makubwa katika umma wake, miogoni mwa walioingia motoni watolewe katika moto, na uombezi huu ni wake na wengineo katika manabii na watu wema.

77 NI VIPI VIGAWANYO VYA KUZURU MAKABURI ?

JIBU: 1) Ziara ya kisheria, nayo ni ziara kwa ajili ya mazingatio na kuwaombea dua waislamu walio kufa .

2)Ziara ya kishirikina, nayo ni kufanya ziara kwa ajili ya kuyaomba makaburi na kumshirikisha Allah katika makaburi na kuyachinjia.

3) Ziara ambayo ni bidaa(uzushi), nayo ni kuyafanyia ziara makaburi kwa ajili ya kumuomba Allah katika makaburi na kukhusisha masiku maalumu kwa ajili ya jambo hilo.

4) Ziara ambayo ni maasiya, nayo ni ile ambayo anaasiwa Allah katika makaburi, kama vile kuchukia kadari na kukithirisha kuyazuru makaburi kwa wanawake.

# TWAHARA NA SWALA

78 NI VIPI VITENGUZI VYA UDHU?

JIBU: 1) Chenye kutoka katika njia mbili(tupu ya nyuma na tupu ya mbele).
2)Usingizi.
3) Tendo la ndoa.
4) kutokwa na akili.
5) kugusa tupu kwa mkono, sawa sawa ikawa ni tupu ya mbele au ya nyuma.
6)Kula nyama ya ngamia.
7) Kukufuru, katika kauli sahihi. Allah atukinge na ukafiri.

وآكِل لحم الجمال يًنقض وخارج من قبل أو دبر
والنوم أو جنابة ومن غمي وردة ذهاب عقل يعترى

Maana ya beti ni; (na kula nyama ya ngamia kunatengua udhu, na chenye kutoka katika tupu ya mbele au nyuma. na usingizi na janaba na mwenye kuzimia, na mwenye kuritadi, na mwenye kuondokwa na akili).

79 NI ZIPI NGUZO ZA UDHU?

JIBU: Ni sita:
1) kuosha uso.
2) kuosha mikono mpaka katika fundo mbili.
3) Kupaka kichwa.
4) Kuosha miguu miwili.
5) Kufuata mpangilio.
6) kufuatanisha.

80 NI ZIPI SHARTI ZA UDHU?

JIBU: 1) Uislamu, nayo ni sharti ya kusihi kila ibada.
2) kutokupatikana kizuizi ambacho kinazuia maji kufika katika ngozi.
3) Akili, hausihi udhu kwa mwenye kichaa.
4) kutakasika kwa mwanamke kutokana na hedhi au janaba.
5) kupatikana maji moja kwa moja.

6) kufikia baleghe.
7) kuweza kutawadha.

81 NI ZIPI SHARTI ZA SWALA?

JIBU: 1) Uislamu.
2)Akili.
3) Utambuzi.
4) Kuondoa hadathi.
5) kustiri uchi.
6) kuondosha najsi.
7)Kuigia wakati.
8) Kuelekea qibla.
9) Niyah.

82 NI ZIPI NGUZO ZA SWALA?

JIBU: 1) Kusimama kwa mwenye uwezo.
2)Takbiratul ihraam(ya mwanzo).
3) kusoma Suratu Al- Faatiha.
4) Rukuu.
5) kuinuka kutoka katika Rukuu.
6) kuitidali(ni kusimama hali ya kuwa umenyooka).
7) kusujudu juu ya viungo saba.
8) kikao baina ya sijida mbili.
9) Kutulizana katika nguzo zote.
10) Kufuata taratibu(mpangilio huu).
11) kusoma Tashahudi ya mwisho.
12) Kikao cha tashahudi ya mwisho.
13) Kumswalia mtume ﷺ.
14) Salamu mbili.

83 NI YAPI MAMBO YA WAJIBU KATIKA SWALA?

JIBU: 1) Takbira zote kutoa Takbiratul-ihramu.
2) Kusema “**Subhaana Rabbiya Al’ Adhimu**” katika rukuu.

3) kusema “**SamiAllaahu Liman Hamidah**” kwa imamu na anaye swali peke yake.
4) Kusema “**Rabbana Walakal-Hamdu**”.
5) kusema “**Subhaana Rabbiya Al’ala**”.
6) kusema “**Rabbigh Firlii**” baina ya sijida mbili.
7) Tashahudi ya mwanzo.
8) kikao chake(Tashahudi).

84 NI IPI NAMNA YA SWALA YA JENEZA?

JIBU: Anatoa takbira ya kwanza, kisha anasoma suratul Faatiha,
- kisha anatoa takbira ya pili na anamswalia mtume ﷺ na bora zaidi asome Swalatu Ibrahimiya,
- Kisha anatoa takbira ya tatu na anamuombea maiti kwa ikhlas, kwa moja ya dua zilizo pokelewa kutoka kwa mtume ﷺ kufanya hivyo inakuwa bora zaidi, na miogoni mwa dua, ni ile aliyoipokea Muslim kutoka kwa Aufu bin Maalik رضي الله عنه amesema, “aliswalia mtume ﷺ jeneza, nikahifadhi katika dua yake na hali yeye akisema,

**«اللهُمَّ، اغْفِرْ لَهُ وَارْحَمْهُ وَعَافِهِ وَاعْفُ عَنْهُ، وَأَكْرِمْ نُزُلَهُ، وَوَسِّعْ مُدْخَلَهُ، وَاغْسِلْهُ بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ، وَنَقِّهِ مِنَ الْخَطَايَا كَمَا نَقَّيْتَ الثَّوْبَ الْأَبْيَضَ مِنَ الدَّنَسِ، وَأَبْدِلْهُ دَارًا خَيْرًا مِنْ دَارِهِ، وَأَهْلًا خَيْرًا مِنْ أَهْلِهِ وَزَوْجًا خَيْرًا مِنْ زَوْجِهِ، وَأَدْخِلْهُ الْجَنَّةَ وَأَعِذْهُ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ - أَوْ مِنْ عَذَابِ النَّارِ»**

“**Ewe Allah msamehe yeye na mrehemu na umpe afya na umpe msamaha, na ukirimu mashukio yake, na upanue maingio yake(katika kaburi), na umuoshe kwa maji na barafu na umande, na umsafishe kutokana na makosa kama inavyosafishwa nguo nyeupe kutokana na uchafu, na umbadilishie nyumba iliyo bora kuliko nyumba yake, na familia bora kuliko familia yake, na mke au mume bora kuliko wake, na umuingize peponi na umkinge na adhabu ya kaburi au na adhabu ya motoni”.**
- na kisha anatoa takbira ya nne,
kisha anatoa salamu kuliyani mwake na kushotoni mwake. Na panafichwa kisomo katika swala ya jeneza wala hakidhihirishwi.

# ZAKA

85 ZAKA NI NINI?

JIBU: ni ziada, nayo ni kutoa sehemu katika mali kwa nia ya kuitakasa mali.

86 NI ZIPI SHARTI ZA UWAJIBU WA ZAKA?

JIBU:

1) Uislamu.
2) Kuwa huru(si mtumwa).
3) kumiliki kiwango cha kutolewa zaka.
4) Kuzungukwa na mwaka.

87 NI ZIPI SAMPULI ZA VITU VINAVYO TOLEWA ZAKA?

JIBU:

1) Dhahabu na Fedha(madini).
2) Chenye kutoka katika ardhi, miongoni mwa nafaka na matunda ambavyo vimejulishwa na sunna kuwa vinatolewa zaka.
3) Wanyama wa mifugo, ambao ni ngamia, ng’ombe, mbuzi au kondoo.

# SWAUMU

88 FUNGA NI NINI?

JIBU: Funga ni kuacha chakula na kinywaji, na tendo la ndoa, kuanzia kuchomoza kwa Al-fajiri ya kweli mpaka kuzama kwa jua.

89 NI YAPI MAMBO YANAYO PENDEZEWA KATIKA FUNGA?

JIBU: 1) Kukithirisha katika kutoa sadaka, na kusoma Qur’ani na kuwafuturisha wafungaji na kukithirisha katika matendo mengine mema kama sadaka.

2) Kuchelewesha Daku, kwa kauli ya mtume ﷺ, “ **kuleni daku hakika katika kula daku kuna baraka**”.

3) kuwahisha kufuturu.

4) kufanya Umra, kwa kauli ya mtume ﷺ, “**Umra katika Ramadhani inalingana na hijja**”.

5) kusema, “**mimi nimefunga**” kwa atakaye kutukana.

90 NI YAPI MAMBO YENYE KUCHUKIZA KATIKA FUNGA?

JIBU: 1) Kuzidisha katika kusukutua na kupandisha maji puani, kwa kauli yake mtume ﷺ “**zidisha katika kupandisha maji puani isipokuwa utakapokuwa umefunga**”.

2) Kubusu, kwa mwenye matamanio makali.

3) Kumeza makohozi.

4) Kuonja chakula pasina ya haja.

91 NI ZIPI NYUDHURU ZENYE KUHALALISHA KUTOKUFUNGA NDANI YA MWEZI WA RAMADHANI?

JIBU: 1) maradhi na uzee.

2) safari, kwa kauli yake Allah mtukufu,

**{فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيضًا أَوْ عَلَى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ} [البقرة: 184]**

**{Na yule mwenye kuwa mgonjwa miongoni mwenu au akawa safarini, basi atimize hisabu katika siku nyingine**}. [Baqara 184]

3) Hedhi na Nifasi, kwa hadithi ya Abuu Said al-Khuduriy ﵁ hakika ya mtume ﷺ Amesema, "**Hivi si huwa anapopata hedhi mwanamke haswali wala hafungi?**".
4) Mwanamke mwenye mimba, au anaye nyonyesha, kwa kile alichokipokea Anas al-Kaaby﵁ amesema, amesema mtume wa Allahﷺ "**Hakika ya Allah amemuondolea msafiri nusu ya swala na funga na amemuondolea mwanamke mwenye mimba na anaye nyonyesha funga**". Na inawawajibikia wao kulipa.

92 NI YAPI MAMBO YENYE KUFUNGUZA SWAUMU?
JIBU: Moja: Kula na kunywa kwa makusudi.
Mbili: Kufanya tendo la ndoa.
Tatu: kujitapisha kwa makusudi.
Nne: Kutokwa na damu ya hedhi au nifasi, na inawajibika kwa mwanamke huyu kulipa. kwa kauli yake mtume ﷺ kwa mwanamke, "**Hivi si kuwa anapopata hedhi mwanamke haswali wala hafungi?**".
Tano: Kunuiya kufugua, basi yoyote mwenye kunuiya kufungua inatenguka funga yake.
Sita: kuritadi, kwa kupingana kwake na Ibada, na kwa kauli yake Allah mtukufu,

**{لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ} [الزمر: 65]**

**{Lau ungeli mshirikisha Allah, zinge poromoka amali zako**}. [Zumar 65].

# HIJJA

93 NI ZIPI NGUZO ZA HIJJA?

JIBU: Hijja ina nguzo nne.

1) Kuhirimia, nako ni kunuiya kuingia katika Ibada ya hijja, kwa kauli ya mtume ﷺ "**Hakika si vinginevyo, matendo ni kutokana na nia**".

2) Kusimama katika viwanja vya Arafa, kwa kauli ya mtume ﷺ "**Hijja ni Arafa, basi yule ambaye amekuja usiku wa Arafa kabla ya kuchomoza kwa Al-fajiri, atakuwa ameidiriki hijja"** Ameipokea Abuu Daud.

3) Kutufu twawaful ifaadhwa(siku ya kuchinja), kwa kauli yake Allah mtukufu,

**{ثُمَّ لْيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ وَلْيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ} [الحج: 29]**

{**Kisha wajisafishe miili yao(kwa kuondoa kucha na nywele), na watekeleze nadhiri zao, na waizunguke Nyumba huru ya Kale**}. [Hajj 29]

4) Kwenda mwendo wa haraka baina ya Swafa na Marwa.

94 NI YAPI MAMBO YA WAJIBU KATIKA HIJJA ?

JIBU: Ama mambo ya wajibu katika hijja ni;

1) Kuhirimia kutoka katika vituo vya kuhirimia.
2) Kulala Muzidalifa usiku wa siku ya kuchinja.
3) Kulala Mina katika masiku matatu, baada ya Iddi.
4) Kurusha vijiwe.
5) Kunyoa au kupunguza nywele.
6) Kutufu twawafu ya kuaga.

95 NI YAPI MAMBO YA SUNNAH KATIKA HAJJI?

JIBU: Kila kisichokuwa nguzo na mambo haya ya wajibu miongoni mwa matendo ya hijja, basi kitu hicho ni sunna na kinapendezewa, kama vile;

- kulibusu jiwe jeusi,
- kutembea mwendo wa haraka kidogo wakati wa kutufu,
- kufunga rubega,
- kuswali katika masimamo(makaamu) ya nabii Ibrahim, na matendo mengineyo ya sunna yaliyothibiti kutoka kwa mtume صلى الله عليه وسلم.

# FAIDA TOFAUTI TOFAUTI.

96 INAFAA KUSIMAMA KWA AJILI YA ASIYE KUWA ALLAH?

JIBU: Haifai kusimama kwa ajili ya mtu, na dalili ni kauli yake Allah mtukufu anasema,

**{وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ} [البقرة: 238]**

{**Na simameni kwa ajili ya Allah hali ya kuwa ni wenye kunyenyekea**} [Baqara 238]

Na katika hadithi ya Muawiya رضي الله عنه amesema, nilimsikia mtume ﷺ akisema, "**mwenye kupenda kusimamiwa na watu, basi na aandae makazi yake motoni**". Amepokea Tirmidhiy.

97 NI MANENO YAPI AMBAYO MTUME ﷺ ALIMFUNDISHA IBN ABBAS رضي الله عنه ?

JIBU: kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه amesema, "nilikuwa nyuma ya mtume ﷺ siku moja akasema, "**ewe kijana hakika mimi ninakufundisha maneno, muhifadhi Allah nae atakuhifadhi, muhifadhi Allah nae utamkuta mbele yako, na pindi utakapo omba basi muombe Allah pekee, na utakapo taka msaada basi mtake msaada Allah, na fahamu ya kuwa lau kama umma wote ungejikusanya ili wakunufuishe kwa kitu, wasingeweza kukunufaisha kwa chochote isipokuwa kwa kitu alicho kuandikia Allah, na lau kama wangejikusanya juu ya kukudhuru kwa kitu chochote wasingeweza kukudhuru kwa kitu chochote isipokuwa kwa kitu alicho kuandikia Allah juu yako, kalamu zimenyanyuliwa na nyaraka zimekauka**" hadithi hii ni sahihi ameipokea Tirmidhiy.

98 NI NINI MTUME ﷺ ALIMFUNDISHA UMAR BIN SALAMAH رضي الله عنه ?

JIBU: Amesema Umar bin Salamah رضي الله عنه nilikuwa kijana mdogo chini ya malezi ya mtume ﷺ na ulikuwa mkono wangu unazunguka katika sahani, akasema mtume ﷺ kuniambia mimi, “**Ewe kijana, mtaje Allah, na kula kwa mkono wako wa kulia na kula chakula kinacho kuelekea**” akasema, haukuacha kuwa huo ndio ulaji wangu baada ya hapo. Ameipokea Bukhari na Muslim.

99 NI UPI WAJIBU WA WAZAZI KWA WATOTO?

JIBU: Wajibu wa wazazi kwa watoto; ni kuwalea juu ya kitabu cha Allah na mwenendo wa mtume ﷺ na juu ya kuwapenda wema wa umma huu walio tangulia, na kuwa fungamanisha na Allah peke yake na kumfuata mtume ﷺ na kuacha kuwaiga wanachuoni na wengineo.

Na dalili ni hadithi ya Ibn Umar رضي الله عنه amesema, amesema mtume wa Allah ﷺ “**Nyote nyinyi ni wachunga, na kila mmoja wenu ni mwenye kuulizwa kuhusiana na raia wake**”. Ameipokea Bukhari na Muslim.

100 NI NINI ANASEMA MUISLAMU ATAKAPO AMKA(SHTUKA) USIKU?

JIBU: Kutoka kwa Ubaadah bin Swaamit رضي الله عنه kutoka kwa mtume ﷺ Amesema, “ **yeyote mwenye kuamka usiku akasema:**

**لاَ إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، الحَمْدُ لِلَّهِ، وَسُبْحَانَ اللَّهِ، وَلاَ إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَاللَّهُ أَكْبَرُ، وَلاَ حَوْلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ،**

“**Hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, ufalme ni wake na sifa nzuri ni zake, naye juu ya kila kitu ni muweza, sifa njema anastahiki Allah, na utakatifu ni wa Allah, hapana mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na Allah ni mkubwa, na wala hakuna hila**

**kwetu yakuacha maasi na wala nguvu ya kufanya twa'a isipokuwa kwa Allah," kisha Akasema ewe Allah nisamehe mimi au akaomba, atajibiwa na ikiwa atatawadha na akaswali itakubaliwa swala yake**". Ameipokea Bukhari(1104)

101 NI NINI ANASEMA ANAPOAMKA KUTOKA USINGIZINI?

JIBU: Kutoka kwa Hudheifa binl Yamaan ﷺ Amesema, alikuwa mtume ﷺ anapotaka kulala Anasema,

«بِاسْمِكَ أَمُوتُ وَأَحْيَا»

«**kwa jina lako ninakufa na ninakuwa hai**». na anapoamka anasema

«الحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا وَإِلَيْهِ النُّشُورُ»

«**Sifa njema zinamstahiki Allah ambaye katupa uhai baada ya kuwa ametufisha, na kwake yeye tutakusanywa**».

102 NI NINI ANASOMA MUISLAMU KATIKA SUNNA YA ALFAJIRI?

JIBU: Anasoma **suratul Faatiha** na **suratul Kaafiruun** katika rakaa ya kwanza, na katika rakaa ya pili anasoma **suratul Faatiha** na **suratul Ikh-laas**.

103 NI NINI ANASOMA MWENYE KUSWALI KATIKA SWALA YA WITRI?

JIBU: Kutoka kwa Abdur-Rahman Ibn Abza kutoka kwa baba yake ﷺ, kutoka kwa mtume ﷺ kwamba yeye alikuwa anasoma katika rakaa ya kwanza katika swala ya witri '**Sabbihisma Rabikal Alaa**' na katika rakaa ya pili anasoma '**suratul Kaafiruun**' na katika rakaa ya tatu anasoma '**Qul-huwa llaahu Ahad'**. Ameipokea Ahmad(15354)

104 NI NINI ANASEMA MWENYE KUTAKA KUINGIA CHOONI?

JIBU: Kutoka kwa Anas ﵁ amesema, “alikuwa mtume ﷺ pindi anapoingia chooni anasema,

«اللهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْخُبْثِ وَالْخَبَائِثِ»

(**Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na masheitwani wa kiume na masheitwani wa kike**)”.

Na katika mapokezi mengine “alikuwa pindi anapotaka ....”. Ameipokea Bukhari (132) na Muslim(375)

105 NI IPI IDADI YA SWALA NA RAKAA ZAKE?

JIBU: Ni Swala tano, usiku na mchana .

Alfajiri ni rakaa mbili, na Adhuhuri ni rakaa nne, na Alasiri ni rakaa nne, na Magharibi ni rakaa tatu, na Ishaa ni rakaa nne.

106 NI NINI ANASEMA MUISLAM ANAPOANZA SWALA ?

JIBU: Anatoa takbira kisha anasoma **suratul faatiha** kwa hadithi ya Ubaada bin Swamit ﵁ amesema, amesema mtume ﷺ “**hana swala yule ambaye hakusoma suratul Faatiha”**. Ameipokea Bukhari na Muslim.

107 NI NINI ANASEMA MWENYE KUSWALI BAADA YA TAKBIRA YA UFUNGUZI WA SWALA?

JIBU: Anasema,

"اللهُمَّ بَاعِدْ بَيْنِي وَبَيْنَ خَطَايَايَ كَمَا بَاعَدْتَ بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ، اللهُمَّ نَقِّنِي مِنْ خَطَايَايَ كَمَا يُنَقَّى الثَّوْبُ الْأَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسِ، اللهُمَّ اغْسِلْنِي مِنْ خَطَايَايَ بِالثَّلْجِ وَالْمَاءِ وَالْبَرَدِ "

(**Ewe Allah weka mbali baina yangu na baina ya makosa yangu kama vile ulivyo weka mbali baina ya mashariki na magharibi, ewe Allah nitakatishe mimi kutokana na makosa kama inavyo takatishwa nguo nyeupe kutokana na madoa, ewe Allah osha makosa yangu kwa barafu na maji na umande**). Na hii ni

hadithi sahihi zaidi katika mlango huu ameipokea Bukhari(744) na Muslim (598) kutoka kwa Abuu Huraira رضي الله عنه .

108 NI NINI ANASEMA MUISLAMU KATIKA RUKUU YAKE ?

JIBU: Anasema katika rukuu yake,

«سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ»

«**Utakasifu ni wa mola wangu aliye mkubwa**» ameipokea Muslim (772) kutoka kwa Hudheifa رضي الله عنه amesema kutoka kwa mtume صلى الله عليه وسلم

Na anasema katika rukuu yake na sujudu yake,

«سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي»

«**Utakasifu ni wako ewe Allah mola watu, na sifa njema ni zako, ewe Allah nisamehe mimi**». Ameipokea Bukhari [761] na Muslim [484] kutoka kwa Aisha رضي الله عنها amesema, "alikuwa mtume صلى الله عليه وسلم anasema katika rukuu yake na sujudu yake ...."

Au anasema,

«سُبُّوحٌ قُدُّوسٌ، رَبُّ الْمَلَائِكَةِ وَالرُّوحِ»

«**Utakasifu utakasifu ni wa mola wa malaika na roho(Jibril)**» Ameipokea muslimu kutoka kwa Aisha رضي الله عنها .

Au anasema,

«سُبْحَانَ ذِي الْجَبَرُوتِ وَالْمَلَكُوتِ وَالْكِبْرِيَاءِ وَالْعَظَمَةِ»

«**Utakasifu ni wa mwenye kuunganisha na mwenye ufalme na kiburi na ukubwa**». Ameipokea Nasaai [1049] kutoka kwa Aufu bin Maalik رضي الله عنه amesema, nilisimama pamoja na mtume صلى الله عليه وسلم usiku mmoja, pindi alipo rukuu alikaa makadirio ya kiasi cha surat **Al-Baqara** anasema katika rukuu yake ....» Na hadithi hii iko katika Sahihi Musnad ya sheikh wetu Al-Wadiiy Allah amrehemu.

109 JE, YAFAA AKAKUSANYA MWENYE KUSWALI DUA HIZI KATIKA RUKUU AU SUJUDU YAKE?

JIBU: ndiyo yafaa,

Na anasema katika sijda,

«سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى»

«**Utakasifu ni wa mola wangu aliye juu**». Ameipokea Muslim [772] kutoka kwa Hudheifa ﵁ kutoka kwa mtume ﷺ

Au anasema pia,

«اللهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي كُلَّهُ دِقَّهُ، وَجِلَّهُ، وَأَوَّلَهُ وَآخِرَهُ وَعَلَانِيَتَهُ وَسِرَّهُ»

«**Ewe Allah nisamehe mimi dhambi zangu zote ndogo na kubwa na za mwanzo na za mwisho na za wazi na zilizo fichikana**» Ameipokea Muslim (483) kutoka kwa Abuu Huraira﵁ hakika ya mtume ﷺ alikuwa akisema katika sijda yake, ....»

110 NI IPI DUA YA KUNYANYUKA KUTOKA KATIKA RUKUU?

JIBU:

«سَمِعَ اللهُ لِمَنْ حَمِدَهُ»

«**Allah amemsikia yule mwenye kumsifu**»**.** dua hii ni kwa Imamu na anaye swali peke yake. Ameipokea Bukhari [722] na Muslim [416] kutoka kwa Abu Huraira ﵁ .

Kisha anasema Imamu na Ma-amuma na mwenye kuswali peke yake.

**«رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ، مِلْءُ السَّمَاوَاتِ وَمِلْءُ الْأَرْضِ، وَمِلْءُ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ، أَهْلَ الثَّنَاءِ وَالْمَجْدِ، أَحَقُّ مَا قَالَ الْعَبْدُ، وَكُلُّنَا لَكَ عَبْدٌ: اللهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ، وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ».**

«**Ewe Allah mola wetu ni zako sifa njema, ujazo wa mbingu na ardhi na kilicho baina yake na ujazo wa kitu ulicho kitaka baada, mwenye kustahiki sifa na utukufu, ni haki kile alicho kisema mja, na sisi wote kwako ni waja, Ewe Allah hakuna**

**mwenye kuzuia ulichokitoa, na wala hakuna mwenye kukitoa ulicho kizuia, na wala hanufaishi mwenye utukufu, kwako wewe ndio kuna utukufu**». Ameipokea Muslim [347] kutoka kwa Abuu Said ﵁ .

Au anasema,

**«رَبَّنَا وَلَكَ الحَمْدُ حَمْدًا كَثِيرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيهِ»**

«**Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema, kusifu kuliko kwingi, kuzuri kwenye baraka ndani**». Ameipokea Bukhari [799] kutoka kwa Rifaa bin Raafii Az-zarqiy﵁ .

111 NI IPI DUA BAINA YA SIJIDA MBILI?

JIBU,

**«رب اغفر لي ».**

«**Ewe mola wangu nisamehe mimi**» ameipokea Darimiy [1324] kutoka kwa Hudheifa ﵁ kwa hakika alikuwa akisema Mtume ﷺ baina ya sijida mbili "**ewe mola wangu nisamehe mimi**".

112 NINI ANASEMA MWENYE KUSWALI KATIKA TASHAHUDI?

JIBU :

**"التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ، السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللهِ الصَّالِحِينَ ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ"**

**"Maamkizi mema ni kwa ajili ya Allah na swala na mambo mazuri, amani iwe juu yako ewe Nabii na rehema za Allah na baraka zake, amani iwe juu yetu na juu ya waja wa Allah wema, nashuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na mtume wake".** Ameipokea Bukhari [831] na Muslim [402] kutoka kwa Abdilaah bin Masuudi﵁ .

113 NI IPI NAMNA YA KUMSWALIA MTUME ﷺ BAADA YA TASHAHUDI?

JIBU: kutoka kwa Kaabi bin Ujra رضي الله عنه amesema, alitutokea sisi mtume ﷺ tukasema kwa hakika tumeshafahamu namna ya kukusalimia wewe, je ni vipi tukuswalie ? akasema semeni,

**"اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ، وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ، وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ "**

**"Ewe Allah mswalie Muhammad na watu wa Muhammad kama vile ulivyo mswalia Ibrahim na watu wa Ibrahim hakika wewe ni mtukufu mwenye kuhimidiwa. ewe Allah mbariki Muhammad na watu wa Muhammad kama ulivyo mbariki Ibrahim na watu wa Ibrahim hakika wewe ni mtukufu mwenye kuhumidiwa"**. Ameipoka Bukhari [3370] na Muslim [406].

114 NI NINI KINASEMWA KABLA YA SALAMU KATIKA SWALA?

JIBU :

**"اللهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ جَهَنَّمَ، وَمِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، وَمِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ، وَمِنْ شَرِّ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَّالِ "**

**1-"Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na adhabu ya jahannam na kutokana na adhabu ya kaburi na kutokana na fitna ya uhai na umauti na kutokana na shari ya masihi Dajjaali"**. Ameipokea Muslim [588] kutoka kwa Abuu Huraira رضي الله عنه amesema, amesema mtume ﷺ "**atakapokaa tashahudi mmoja wenu basi ajikinge kwa Allah kutokana na mambo manne, aseme " ewe Allah ....**".

**"اللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي ظُلْمًا كَثِيرًا، وَلاَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ، فَاغْفِرْ لِي مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ، وَارْحَمْنِي إِنَّكَ أَنْتَ الغَفُورُ الرَّحِيمُ "**

**2-"Ewe Allah hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu dhulma nyingi na wala hamna mwenye kusamehe madhambi isipokuwa wewe, nisamehe mimi msamaha kutoka kwako na unirehemu, hakika wewe ni mwingi wa kusamehe na mwingi**

**wa kurehemu"**. Ameipokea Bukhari [834] na Muslim [2705] kutoka Abdillah bin Amur ﷺ kutoka kwa Abuu Bakari ﷺ hakika yeye alimwambia mtume ﷺ "nifundishe dua ambayo nitaomba kwa dua hiyo katika swala yangu" mtume akasema kumwambia Abuu bakar ﷺ sema, "**Ewe Allah ....**"

115 NINI KINASEMWA WAKATI WA KUTOKA KATIKA SWALA, NA NI IPI NAMNA YA KUTOA SALAMU?

JIBU:

**«السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ »**

«**Amani na rehma za Allah ziwe juu yenu**» Kulia na kushoto. ameipokea Ahmad [3699] kutoka kwa Abdillah ﷺ hakika ya mtume ﷺ alikuwa akitoa salamu upande wake wa kulia na upande wake wa kushoto mpaka unaonwa weupe wa shavu lake. na sanadi ya hadithi hii ni sahihi.

116 NI IPI SUNNA KATIKA KUREFUSHA SWALA?

JIBU: Sunna ni arefushe katika swala ya Alfajiri, kisha Adh-dhuhur kisha Alasiri kisha Magharibi kisha Ishaa,

Na anarefusha katika rakaa ya kwanza na anapunguza katika rakaa inayofuata baada yake na wala imamu asirefushe sana mpaka akawapa uzito watu(ma-amuma).

117 NINI ANASEMA MUISLAMU ATAKAPO SHUKA KATIKA KITUO(SEHEMU)?

JIBU : Anasema

**«أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ»**

«**Ninajikinga kwa maneno ya Allah yaliyokamilika, kutokana na shari ya vile alivyoviumba**».

118 NI IPI DUA YA KUINGIA NYUMBANI?

JIBU:

**بِسْمِ اللَّهِ**

**«Kwa jina la Allah».**

119 NINI ANASEMA MUISLAMU WAKATI WA KUMALIZA KULA?

JIBU: Anasema

**الحمد لله**

Kutoka kwa Anas bin Maalik ﵁ amesema, amesema Mtume ﷺ "**hakika ya Allah anamridhia mja anapokula chakula kisha akamuhimidi kwa chakula hicho, au akanywa kinywaji kisha akamuhimidi kwa kinywaji hicho**". ameipokea Muslim {2734}

120 TAJA WALIOHARAMISHWA KUOLEWA KATIKA WANAWAKE AMBAO INAFAA KUWAANGALIA NA KUWAPA MKONO?

JIBU: Ni mama yako, binti yako, dada yako, binti wa mtoto wako wa kiume au wa kike, binti wa dada au kaka, na mwanamke aliye kunyonyesha, dada uliyenyonya nae, mke wa mtoto wako, mama wa mke, na mtoto wa mkeo uliyemuoa.

Amesema Allah mtukufu,

**{حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ الْأَخِ وَبَنَاتُ الْأُخْتِ وَأُمَّهَاتُكُمُ اللَّاتِي أَرْضَعْنَكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ مِنَ الرَّضَاعَةِ وَأُمَّهَاتُ نِسَائِكُمْ وَرَبَائِبُكُمُ اللَّاتِي فِي حُجُورِكُمْ مِنْ نِسَائِكُمُ اللَّاتِي دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَإِنْ لَمْ تَكُونُوا دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا} [النساء: 23].**

{**Mmeharimishiwa mama zenu, na binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na khaalati(mama wakubwa au wadogo) zenu, na binti wa kaka, na binti wa dada, na mama zenu walio kunyonyesheni, na dada zenu kwa kunyonya, na mama wa wake zenu, na watoto wa kambo walio katika ulinzi wenu walio zaliwa na wake zenu mlio waingilia. Ikiwa hamkuwaingilia basi hapana lawama juu yenu. (Pia mmeharimishwa) wake wa watoto wenu walio toka katika migongo yenu. Na kuwaoa pamoja dada wawili isipo kuwa yale yaliyo kwisha pita.**

**Hakika Allah ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu**}. [Nisaa 23]. Na wala haifai kuchanganyika na wasio kuwa hao na kuwapa mikono.

121 NI NANI MBORA WA WATU BAADA YA MTUME ﷺ ?

JIBU: Mbora wao baada yake ni Abuu Bakari kisha Umar kisha Uthmaan kisha Ally kisha maswahaba kumi walio bashiriwa pepo رضي الله عنهم .

122 NI AKINA NANI MAKHALIFA WANNE ?

JIBU :- Ni Abuu Bakari Abdillaah bin Uthmaan رضي الله عنه .

- Umar bin Khatwab Abuu Hafswi رضي الله عنه .

- Uthmaan bin Afaan Abuu Abdillaah رضي الله عنه .

- Ally bin Abii Twaalib Abul Hassan رضي الله عنه .

123 NI AKINA NANI MASWAHABA KUMI WALIO BASHIRIWA PEPO?

JIBU: Kutoka kwa Abdur-Rahmaan bin Auf رضي الله عنه hakika ya mtume ﷺ amaesema, “**Abuu Bakar ni mtu wa peponi, na Umar ni mtu wa peponi na Ally ni mtu wa peponi na Uthmaan ni mtu wa peponi na Twalha ni mtu wa peponi na Zubeir bin Awaam ni mtu wa peponi na Abdur-Rahmaan bin Auf ni mtu wa peponi na Said bin Zaid ni mtu wa peponi na Abuu Ubaida binl Jarraah ni mtu wa peponi**”. ameipokea Ahmad.
Amesema Abuu Daud Assijistaany,

**وإنهـم للرهــط لا ريـــب فـيهـم على نجـب الفردوس بروح تسـرح**
**سعيد وسعد وابن عوف وطلحة وعــامر فهـر والـزبيـر الممـــدح**

Maana ya ubeti ni; Hakika wao ni kundi hapana shaka kwao wao, juu ya mito ya firdaus kwa nuru roho zao ni zenye kwenda na kurudi.

Saidi na Saad na mtoto wa Auf na Twalha, na A`mir Fihrin na Zubeir mwenye kusifiwa.

Na walio bashiriwa pepo ni wengi, lakini hawa walitajwa katika kikao kimoja, na miongoni mwa walio bashiriwa pepo wasio kuwa hawa ni **Ukkaasha** na **wake za mtume**ﷺ na **Fatwima** na **Hassan** na **Hussein** na **maswahaba wote**, kama alivyo sema Allah mtukufu,

{وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ } التوبة: [١٠٠]

{**Na wale walio tangulia wa mwanzo, katika Muhaajirina na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Allah ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito chini yake, ni wenye kudumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa**}. [Tauba 100]

124 NI AKINA NANI WANAFIQ’HI SABA WA MJI WA MADINA ?

JIBU: Wamewaandika katika ubeti baadhi ya wanazuoni kwa kauli yao,

إذا قيل من في العلم سبعة أبحر روايتهم ليست عن العلم خارجه
فقل هم عبيد الله عروة قاسم سعيد أبو بكر سليمان خارجه

Maana ya ubeti huu; Utakapo ulizwa ni akina nani bahari saba katika elimu, riwaya zao katika elimu si zenye kutoka.
Basi sema ni Ubeydullah, Urwah, Qaasim, Said, Abuu Bakri, Sulaiman na Khaarija.

Hawa ndio wanafiqhi wa mji wa madina. Majina yao ni;
- Ubaydullah bin Abdillah bin Utba bin Masuud kutoka katika kabila la Hudheir.
- Na Urwa bin Zubeir.
- Na Qaasim bin Muhammad bin Abuu Bakari As-widiq.
- Na Said bin Musayyab kutoka katika wana wa Makh-zuumi.

- Na Abuu Bakri bin Abdur Rahmaan bin Haarith bin Hashim, babu yake Haarith bin Hashim, ni ndugu wa Abuu Jahali kutoka kwa wana wa makh-zuumi.
- Na katika watumwa huru ni Suleiman bin Yasaar na Khaarijah bin Zaid bin Thaabit kutoka katika Maanswari.

125 NI AKINA NANI MA-ABAADILA?

JIBU: Ni

والبحــر وابنـا عُمَــر وعمـرِو وابـن الزبيـر فـي اشتهــار يجــري

Maana ya ubeti ni; Na bahar(Ibn Abaas) na Ibn Umar na Ibn am'ru na Ibn Zubeir katika umaarufu inapita.

126 NI AKINA NANI MASWAHABA WALIO KITHIRISHA RIWAYA KUTOKA KWA MTUME ﷺ?

JIBU: ni,

والمكثـرون فـي روايــة الأثــر أبــو هريــرة يليــه ابــن عمــر

وأنــس والحــبــر كـالـخــدري وجــابــر وزوجــة الـنـبــي

Maana ya ubeti ni; Walio kithirisha katika kupokea athari(kutoka kwa mtume ﷺ ), ni Abuu Huraira na anafuatia Ibn Umar,

Na Anas na Ibn Abbaas na khuduriy(Abuu Said), na Jaabir na mke wa mtume ﷺ

127 NI AKINA NANI WAKE ZA MTUME ﷺ ?

JIBU: 1. Khadiija binti khuweylid رضي الله عنها.

2. Sauda binti Zam'aa رضي الله عنها.

3. Aisha binti Abdillah رضي الله عنها.

4. Hafswa binti Umar رضي الله عنها.

5. Zainabu binti Jahshi رضي الله عنها.

6. Ummu Salama Hindu binti Abi Umeiya رضي الله عنها.

7. Juweiriyya binti Haarith رضي الله عنها.
8. Ramla binti Abi Sufiyani رضي الله عنها.
9. Swafiya binti Huyay رضي الله عنها.
10. Maymuna binti Haarith رضي الله عنها.

ترتيبُ أزواج النبي الهادي     على الذي قد جاءنا في الزاد
بدءُ النكاحِ بخديجةَ اعتُبر     سودةُ عائش كذا بنت عمر
بنت خزيمةَ فهندٌ زينب     فبنت حارث فرملةَ اكتبوا
ميمونةٌ فهذه بها انتهت     وقيل زد ريحانةٌ وما ثبت
مارية أعني بها القبطية     لم يذكروا لأنها سرية.

Maana ya beti hizi ni; Mpangilio wa wake za mtume mwongozaji, juu ya kile kilicho tuijia katika Zaadi(kitabu),
Ndoa ya mwanzo ni kwa Khadiija imezingatiwa, Sauda, Aisha vile vile binti wa Umar,
Binti Khuzaimah kisha Hindu, Zainab kisha binti Haarith kisha Ramla andikeni,
Maymuna kwa huyu ndiyo alikomea, pamesemwa alizidisha Rihaana na haikuthibiti,
Mariya namkusudia Qibtwiya hawakumtaja kwa sababu yeye ni mtumwa.

128 NI AKINA NANI WASHAIRI WA MTUME صلى الله عليه وسلم ?

JIBU: Ni

وشعراء المصطفى ذوو الشان     ابن رواحة وكعب حسان

Maana ya ubeti huu; Na washairi wa mwenye kuchaguliwa wenye hadhi, ni Ibn Rawaaha na Kaabu na Hassan.

129 NI AKINA NANI WAADHINI WA MTUME صلى الله عليه وسلم?

JIBU: Ni Abdillah Ibn Ummi Maktuum, Bilali bin Rabaaha na Abuu Mah-dhuura.

130 NI AKINA NANI MAIMAMU WANNE?

JIBU: Ni - Abuu Abdillah Ahmad bin Hambbal Ash-shaybaaniy.

- Abuu Abdillah Muhammad bin Idriisa Ash-shaafiy.

- Abuu Abdillah Maalik bin Anas Al-Asbuhiy.

- Abuu Hanifa Nuumani bin Thaabit.

131 NI AKINA NANI WATU(MAIMAMU) WA VITABU SITA?

JIBU: **Bukhari**: Abuu Abdillah Muhammad bin Ismail bin Ibrahim bin Bardizba Al-Juufiy. Alikufa mwaka [256 hijr].

**Muslim**: Ibn Hajjaaj bin Muslim Abul Hussein Al-Qushairy An-Naisabuuriy. Alikufa mwaka [261 hijr].

**Abuu daud**: Sulaimaan bin Ash-ath As-sajistaniy. Alikufa mwaka [275 hijr].

**Tirmidhiy**: Abuu Issa Muhammad bin Issa bin Saurah. Alikufa mwaka [279 hijr].

**Nasaaiy**: Abuu Abdur Rahmaan Ahmad bin Shuaib Al-Khurasaaniy. Alikufa mwaka [303 hijr].

**Ibn Maajah**: Abuu Abdillah Muhammad bin Yaziid Al-Qazwiiniy. Alikufa mwaka [283 hijr].

132 NI ZIPI NYIRADI ZA ASUBUHI NA JIONI?

JIBU: ni;
**«اللهمَّ أَنْتَ رَبِّي لا إِلَهَ إلا أَنْتَ خَلَقْتَنِي وَأَنَا عَبْدُكَ وَأَنَا عَلَى عَهْدِكَ وَوَعْدِكَ مَا اسْتَطَعْتُ أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا صَنَعْتُ أَبُوءُ لَكَ بِنِعْمَتِكَ عَلَيَّ وَأَبُوءُ لَكَ بِذَنْبِي فَاغْفِرْ لِي فَإِنَّهُ لا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إلا أَنْتَ»**
«Ewe Allah, wewe ni mola wangu hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe, umeniumba mimi na mimi ni mja wako, na mimi niko juu ya ahadi yako na miadi yako kwa kadri

niwezavyo, najikinga kwako kutokana na shari ya nilichokifanya, na ninakiri neema yako juu yangu na ninakiri dhambi yangu kwako, nisamehe mimi, hakika hakuna anaesamehe madhambi isipokuwa wewe».

Amesema mtume ﷺ "**mwenye kutamka hayo wakati wa mchana, hali ni mwenye yakini nayo, kisha akafa katika siku yake hiyo kabla hajafikiwa na jioni, basi yeye ni mtu wa peponi. na mwenye kuyatamka wakati wa usiku hali ni mwenye yakini nayo, kisha akafa katika usiku wake huo kabla hajafikiwa na asubuhi, basi yeye ni mtu wa peponi**". Ameipokea Bukhari kutoka kwa Shaddad bin Ausi رضي الله عنه [6306].

**«أَمْسَيْنَا وَأَمْسَى الْمُلْكُ لِلَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ لا إِلَهَ إِلا اللَّهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ. لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ رَبِّ أَسْأَلُكَ خَيْرَ مَا فِي هَذِهِ اللَّيْلَةِ وَخَيْرَ مَا بَعْدَهَا وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا فِي هَذِهِ اللَّيْلَةِ وَشَرِّ مَا بَعْدَهَا رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ الْكَسَلِ وَسُوءِ الْكِبَرِ رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابٍ فِي النَّارِ وَعَذَابٍ فِي الْقَبْرِ»**

«Tumefikiwa na jioni na umekuwa ufalme ni wa Allah na sifa njema zinamstahiki Allah, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake hana mshirika. ni wake yeye ufalme na ni zake yeye sifa njema, naye juu ya kila kitu ni muweza, ewe mola wangu nakuomba kheri iliyo ndani ya usiku huu na kheri iliyo baada yake, na ninajikinga kwako kutokana na shari iliyo ndani ya usiku huu na shari iliyo baada yake, ewe mola wangu najikinga kwako kutokana na uvivu na ukubwa(uzee) mbaya na ninajikinga kwako kutokana na adhabu katika moto na adhabu katika kaburi».

Na anapofikiwa na asubuhi anasema, "**tumefikiwa na asubuhi....)** ameipokea Muslim [2723] kutoka kwa Ibn Masuud رضي الله عنه .

**« بِسْمِ اللَّهِ الَّذِي لا يَضُرُّ مَعَ اسْمِهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلا فِي السَّمَاءِ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ »**

«Kwa jina la Allah ambaye hakidhuru kitu pamoja na jina lake katika ardhi wala mbinguni, nae ni msikivu na mjuzi» (mara tatu) mwenye kusema dua hii hakitomdhuru kitu chochote. Ameipokea Abuu Daud [5088]. na hadithi hii iko katika Sahihi Musnad ya Imamu Al-waadiy Allah amrehemu.

«اللَّهُمَّ بِكَ أَصْبَحْنَا وَبِكَ أَمْسَيْنَا وَبِكَ نَحْيَا وَبِكَ نَمُوتُ وَإِلَيْكَ النُّشُورُ ،وَإِذَا أَمْسَى. فَلْيَقُلْ: اللَّهُمَّ بِكَ أَمْسَيْنَا وَبِكَ أَصْبَحْنَا وَبِكَ نَحْيَا وَبِكَ نَمُوتُ وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ»

«Ewe Allah kwa msada wako tumefikiwa na asubuhi na kwa msaada wako tumefikiwa na jioni na kwa msaada wako tunakuwa hai na kwa msaada wako tunakufa na kwako wewe tutakusanywa». Na anapofikiwa na jioni anasema, «Ewe Allah kwa msada wako tumefikiwa na jioni na kwa msaada wako tumefikiwa na asubuhi na kwa msaada wako tunakuwa hai na kwa msaada wako tunakufa na kwako wewe ndio kuna marejeo». Ameipokea Abuu Daud kutoka kwa Abuu Huraira ﵁ [5068].

«اللَّهُمَّ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ عَالِمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ لا إِلَهَ إِلا أَنْتَ رَبَّ كُلِّ شَيْءٍ وَمَلِيكَهُ أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ نَفْسِي وَمِنْ شَرِّ الشَّيْطَانِ وَشِرْكِهِ وَأَنْ أَقْتَرِفَ عَلَى نَفْسِي سُوءًا أَوْ أَجُرَّهُ إِلَى مُسْلِمٍ»

«Ewe Allah muumba wa mbingu na ardhi, mjuzi wa mambo yaliyo fichikana na yaliyo wazi, hapana mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe, mola wa kila kitu na mmiliki wake, najikinga kwako kutokana na shari ya nafsi yangu na kutokana na shari ya shaitwani na washirika wake na ninajikinga kwako kutokana na kuichumia nafsi yangu ubaya, au kuupeleka kwa muislamu». Ameipokea Ahmad kutoka kwa Abuu Huraira ﵁ na hadithi hii ipo katika Jaamiu Swahihi [2/533] na Swahiha [63].

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَافِيَةَ فِي الدُّنْيَا وَالآخِرَةِ اللَّهُمَّ إني أَسْأَلُكَ الْعَفْوَ وَالْعَافِيَةَ فِي دِينِي ودنياي وأهلي وَمَالِي اللَّهُمَّ اسْتُرْ عَوْرَاتِي وَآمِنْ رَوْعَاتِي اللَّهُمَّ احْفَظْنِي مِنْ بَيْنِ يَدَي وَمِنْ خَلْفِي وَعَنْ يَمِينِي وَعَنْ شِمَالِي وَمِنْ فَوْقِي وَأَعُوذُ بِعَظَمَتِكَ أَنْ أُغْتَالَ مِنْ تَحْتِي»

«Ewe Allah nakuomba afya duniani na akhera, ewe Allah hakika mimi nakuomba msamaha na Afya katika dini yangu na dunia yangu na familia yangu na mali yangu, ewe Allah sitiri uchi wangu na niaminishe hofu yangu, ewe Allah nihifadhi mimi mbele yangu na nyuma yangu na kuliani kwangu na kushotoni kwangu na juu yangu na ninajikinga kwa utukufu wako kutokana na kuzungukwa chini yangu». Ameipokea Abuu Daud [5045] kutoka kwa Ibn Umar ﵄ na wameisahihisha mashekhe wawili Al-waadiy katika Swahihi Musnad na Shekhe Al-baan.

**« أصبحت أثني عليك حمدًا وأشهد أن لا إله إلا الله »**. **وإذا أمسى قال أمسيت...).**
«Nimepambazukiwa hali ya kuwa nakusifu wewe na ninashuhudia kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah». (mara tatu) na anapofikiwa na jioni anasema, " **nimefikiwa na jioni ….**). Ameipokea Nasaaiy [6/147] na hadihti hii iko katika Swahihi Musnad ya Shekhe Muq'bil Allah amrehemu.

«**سبحان الله وبحمد**» (مائة مرة)
«Utakasifu ni wa Allah na kuhimidiwa ni kwake» [mara mia moja(100)] "**mwenye kusema hivi pindi anapofikiwa na asubuhi na pindi anapofikiwa na jioni, hatokuja yeyote siku ya kiyama na bora zaidi ya kile alicho kuja nacho, isipokuwa atakaekuwa amesema mfano wake au kazidisha**". Ameipokea Muslim kutoka kwa Abuu Huraira ﵁ [2691].

«**لا إِلَهَ إِلا اللَّهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ**».
«Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake hana mshirika, ni wake ufalme na ni zake sifa njema naye juu ya kila kitu ni muweza». [mara mia moja(100)] "**mwenye kusema dua hii katika siku yake anakuwa na usawa wa kuacha huru watumwa kumi na ataandikiwa mema kumi na atafutiwa makosa kumi na itakuwa ni kinga yake kutokana na shaitwani kwa siku yake hiyo mpaka afikiwe na jioni na hatokuja yeyote na bora ya kile alicho kuja nacho isipokuwa aliyefanya zaidi ya hivyo**". Ameipokea Bukhari na Muslim kutoka kwa Abuu Huraira ﵁ .

"**Au anaisema mara kumi(10)**" ameipokea hiyo Abuu Daud [5080] kutoka kwa Abuu Ayyaashi ﵁ na ameipokea Ahmad [5/420] kutoka kwa Abuu Ayyub Al-Answaari ﵁ .

«**أَصْبَحْنَا عَلَى فِطْرَةِ الإِسْلاَمِ وَعلى كَلِمَةِ الإِخْلاَصِ وَعلى وَدِينِ نَبِيِّنَا مُحَمَّدٍ وَعلى مِلَّةِ أَبِينَا إِبْرَاهِيمَ حَنِيفاً مُسْلِماً** ».
«Tumepambazukiwa juu ya umbile la uislamu na juu ya tamko la ikhlaswi na juu ya dini ya nabii wetu Muhammad na juu ya mila ya baba yetu Ibrahim mwenye kujiweka mbali na ushirikina mwenye

kujisalimisha». na anapofikiwa na jioni anasema, “**tumefikiwa na jioni ….**” kutoka kwa Abdur-Rahman bin Abza ﵁ ameipokea Ahmad[3/306].

«المعوذات قل هو الله أحد وقل أعوذ برب الفلق وقل أعوذ برب الناس»

Kusoma Muawidhaati(**Qulhuwa Llaahu Ahad, Qul Audhu Bi Rrabil Falaq, Qul Audhu Bi Rrabbin Nnasi**) [mara tatu tatu] ameipokea Ahmad[37/335] na Nasaaiy kwa isnadi iliyo nzuri na ameihasanisha hadithi hii shekhe Al-bany Allah amrehemu.

«سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ عَدَدَ خَلْقِهِ وَرِضَا نَفْسِهِ وَزِنَةَ عَرْشِهِ وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ»

«Utakasifu ni wa Allah na kuhimidiwa ni kwake, idadi ya viumbe vyake na ridhaa ya nafsi yake na pambo la arshi yake na wino wa maneno yake». [mara tatu asubuhi] kutoka kwa Juweiriyya ﵂ . Ameipokea Muslim[6768].

«أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ »

«Najikinga kwa maneno ya Allah yaliyo kamilika kutokana na shari ya alicho kiumba».[mara moja jioni] hakitomdhuru kitu. ameipokea Muslim kutoka kwa Abuu Huraira ﵁ [2709].

«الآيتان من آخر سورة البقرة»

Kusoma aya mbili za mwisho wa Suratul Baqara, “**mwenye kuzisoma aya hizo katika usiku wake zitamtosheleza**”. Ameipokea Bukhari na Muslim kutoka kwa Abuu Masuud Al-Answary ﵁ .

133 NI ZIPI NYIRADI ZA BAADA YA SWALA YA FARADHI ZILIZOTHIBITI KUTOKA KWA MTUME ﷺ ?

JIBU;

«أَسْتَغْفِرُ الله أَسْتَغْفِرُ الله أستغفر الله اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَمِنْكَ السَّلَامُ تَبَارَكْتَ ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ»

1-«Namtaka msamaha Allah, namtaka msamaha Allah, namtaka msamaha Allah. Ewe Allah wewe ni salamu na kwako wewe inatoka amani, umetukuka ewe mwenye utukufu na ukarimu».

Kutoka kwa Thauban ﷺ amesema, alikuwa mtume ﷺ anapotoka katika swala yake, Anataka msamaha mara tatu na anasema, “**Ewe Allah wewe ni salamu** ....” Ameipokea Muslim [931].

«التَّكْبِيرِ»

2- Kuleta Takbira, ameipokea Bukhari na Muslim, kutoka kwa Ibn Abbas ﷺ amesema, nilikuwa nafahamu kumalizika kwa swala ya mtume ﷺ kwa kuleta Takbira.

«آيَةَ الْكُرْسِيِّ (اللهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ... )

3- Kusoma Ayatul Kursiy, kutoka kwa Abuu Umama ﷺ ameipokea Tirmidhiy. “**mwenye kuisoma aya hii baada ya kila swala, hakitokuwa baina yake na baina ya pepo isipokuwa mauti**”.

«قراءة المعوذات. وهي{قل أعوذ بربِّ الناس} و{قل أعوذ بربِّ الفلق}.

4- Kusoma Muawidhaat, ameipokea Abuu Daud[1302] kutoka kwa Uqba bin A`mir ﷺ kutoka kwa mtume ﷺ.

Nazo Muawidhaat ni “**Qul Audhu bi Rabbil Falaq**” na “**Qul Audhu bi Rabbi Nnasi**”.

«لَا إِلَهَ إِلَّا اللهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ اللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ».

5- «Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake hana mshirika ni wake yeye ufalme na sifa njema, naye juu ya kila kitu ni muweza. Ewe Allah hakuna mwenye kuzuia kile ulicho kitoa, na wala hakuna mwenye kutoa kile ulicho kizuia, na wala haimnufaishi mwenye utukufu, kwako wewe ndio unatoka utukufu». Ameipokea Bukhari na Muslim, kutoka kwa Mughiira Ibn Shuuba ﷺ hakika ya mtume ﷺ alikuwa akisema kila baada ya kila swala, “**Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah** ....”

«لَا إِلَهَ إِلَّا اللهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ لَا إِلَهَ إِلَّا اللهُ وَلَا نَعْبُدُ إِلَّا إِيَّاهُ لَهُ النِّعْمَةُ وَلَهُ الْفَضْلُ وَلَهُ الثَّنَاءُ الْحَسَنُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ»

6- «Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake hana mshirika na ni wake ufalme na sifa njema ni zake, nae juu ya kila kitu ni muweza, hakuna hila ya kuacha maasi, wala nguvu ya kufanya twa'a isipokuwa kwa Allah, na wala hatumuabudu isipokuwa yeye, ni zake neema na fadhila na ni zake sifa nzuri, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah hali ya kumtakasia yeye dini na lau watachukia makafiri». kutoka kwa Ibn Zubeir ﵁ amesema alikuwa mtume ﷺ anafanya **Tahalili** kwayo. ameipokea Muslim [594]

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ الْجُبْنِ وَأَعُوذُ بِكَ أَنْ أُرَدَّ إِلَى أَرْذَلِ الْعُمُرِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الدُّنْيَا وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ»

7- «Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na uwoga na ninajikinga kwako kutokana na kurudishwa katika umri wa uzee, na ninajikinga kwako kutokana na fitna za dunia na ninajikinga kwako kutokana na adhabu ya kaburi». ameipokea Bukhari[2822] kutoka kwa Saad ﵁ kwa hakika yeye aliwafundisha watoto wake maneno haya, na akasema hakika ya mtume ﷺ alikuwa anajikinga kwayo baada ya swala.

«رَبِّ قِنِي عَذَابَكَ يَوْمَ تَبْعَثُ عِبَادَكَ ( أَوْ قال : تَجْمَعُ) »

8- «Ewe mola wangu nikinge mimi na adhabu yako siku utakapofufua waja wako (au alisema utakapo wakusanya)». ameipokea Muslim [709] kutoka kwa Al-baraa ﵁ amesema, tulikuwa pindi tunapo swali nyuma ya mtume ﷺ tunapendelea kuwa kuliani mwake, anatuelekea kwa uso wake, amesema Baraa ﵁, "basi nilimsikia akisema maneno haya"

«اللَّهُمَّ أَعِنِّي عَلَى ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَحُسْنِ عِبَادَتِكَ»

9- «Ewe Allah nisaidie mimi juu ya kukutaja wewe na kukushukuru wewe na uzuri wa kukuabudia wewe». Ameipokea Abuu Daud [1301] kutoka kwa Muadh bin Jabal ﵁ hakika ya

mtumeﷺ alichukuwa mkono wake na akasema, "**ninakuusia ewe Muadh usiache kila baada ya swala kusema ….**" akaitaja hadithi hii.

«سُبْحَانَ اللَّهِ. وَالْحَمْدُ لِلَّهِ . وَاللهُ أَكْبَرُ »

10- « Subhana Llahi na Al-hamdu Lillahi na Allahu Akbar» . Mpaka ifikie kila moja mara thelathini na tatu(33) kutoka kwa Abuu Huraira رضي الله عنه kutoka kwa mtume ﷺ ameipokea Bukhari [798] na Muslim.

ويقول تَمَامَ الْمِائَةِ «لَا إِلَهَ إِلَّا اللهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

11- Na anasema kukamilisha mia moja, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake, hana mshirika, nae juu ya kila kitu ni muweza. "**Atasamehewa makosa yake hata kama yatakuwa mfano wa povu la bahari**". kutoka kwa Abuu Huraira رضي الله عنه kutoka kwa mtumeﷺ, Ameipokea Muslim [939].

«سبحان الله (خمسًا وعشرين) والحمد الله (خمسًا وعشرين) والله أكبر (خمسًا وعشرين) ولا إله إلا الله (خمسًا وعشرين)»

12- Subhana Llah(mara ishirini na tano) na Al-hamdu Lillahi(mara ishirini na tano) na Allahu Akbar (mara ishirini na tano) Na Laa Ilaaha Illa Llahu(mara ishirini na tano). Ameipokea Nasaaiy [1333] kutoka kwa Zaid bin Thaabit رضي الله عنه amesema, waliamrishwa walete Tasbihi kila baada ya swala, mara thelathini na tatu na wamuhimidi Allah mara thelathini na tatu na watoe Takbira mara thelathini na nne. Basi akajiwa mtu moja miongoni mwa Maanswari katika usingizi wake, akaambiwa, amekuamrisheni mtume wa Allahﷺ mfanye Tasbihi kila baada ya swala mara thelathini na tatu na mumhimidi Allah mara thelathini na tatu na mtoe Takbira mara thelathini na nne? akasema ndiyo. Akaambiwa, basi zijaalieni ziwe ishirini na tano na jaalieni ndani yake Tahlili(Laa Ilaaha Illa llahu). Pindi alipo pambazukiwa alimwendea mtumeﷺ akamtajia hilo akasema, "**basi zijaalieni hivyo**".

«الله أكبر (عَشْرًا) وَسبحان الله (عَشْرًا) وَالحمد لله (عَشْرًا)

13- «Allahu Akbar (mara kumi) na Subhana Llah (mara kumi) na Al-hamdu Lillahi(mara kumi)» . kutoka kwa Anas bin Maalik ﵁ hakika ya mtumeﷺ alimwambwia Ummu Sulaim ﵂, "**Ewe Ummu Sulaim, pindi utakapomaliza swala ya faradhi sema …. Akaitaja hadithi**" Kisha akasema, "**kisha omba unachotaka, hakika yeye(Allah) anakwambia wewe "ndiyo".** mara tatu. Ameipokea Tirimidhiy[443] na ameipokea Abuu Yaala Al-Muuswily [327].

134 NI ZIPI NYIRADI ZA KULALA ZILIZO THIBITI KUTOKA KWA MTUMEﷺ?

JIBU;

1- Ayatul Kursiy, kutoka kwa Abuu Huraira ﵁ ameipokea Bukhari.

2- Anapuliza katika mikono yake kisha anasoma "**Qul Huwa Llaahu Ahad"** na **"Qul Audhu Bi Rabbil Falaq"** na **"Qul Audhu Bi Rabbi Nnasi"** katika mikono yake, kisha anapakaa sehemu anayoiweza katika mwili wake na anaanzia juu ya kichwa na uso wake na mwili wake kwa mbele, anafanya hivyo(mara tatu). Ameipokea Bukhari kutoka kwa Aisha ﵂, "hakika ya mtumeﷺ alikuwa pindi anapoliendea tandiko lake kila usiku, anakusanya viganja vyake kisha anapuliza katika viganja vyake na anazisoma hizo sura katika viganja vyake …… "

«بِاسْمِكَ اللهم أَمُوتُ وَأَحْيَا. وَإِذَا قَامَ قَالَ: الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا وَإِلَيْهِ النُّشُورُ»

3- «Kwa jina lako ewe Allah nakufa na ninakuwa hai» na anapoamka anasema «sifa njema zina msitahiki Allah ambaye ametupa uhai baada ya kutufisha na kwake yeye tutakusanywa». kutoka kwa Hudheifa binl Yamaan ﵁ [6960] na Abuu Dharri ﵁ [5837] amezipokea Bukhari na Muslim [4886] kutoka kwa

Al-Baraa رضي الله عنه wamesema, “alikuwa mtume ﷺ pindi anapoliendea tandiko lake, anasema ……” mpaka mwisho.

**«اللهمَّ أَسْلَمْتُ نَفْسِي إِلَيْكَ وَوَجَّهْتُ وَجْهِي إِلَيْكَ وَفَوَّضْتُ أَمْرِي إِلَيْكَ وَأَلْجَأْتُ ظَهْرِي إِلَيْكَ رَغْبَةً وَرَهْبَةً إِلَيْكَ لَا مَلْجَأَ وَلَا مَنْجَا مِنْكَ إِلَّا إِلَيْكَ آمَنْتُ بِكِتَابِكَ الَّذِي أَنْزَلْتَ وَبِنَبِيِّكَ الَّذِي أَرْسَلْتَ»**

4- «Ewe Allah nimeisalimisha nafsi yangu kwako na nimeelekeza uso wangu kwako na nimeliegemeza jambo langu kwako na nimeegemeza mgongo wangu kwako hali ya kukupenda na kukuogopa wewe, hapana marejeo wala sehemu ya kukimbilia kutoka kwako isipokuwa kwako, nimeamini kitabu chako ambacho umekiteremsha na nabii wako ambaye umemtuma». “**mwenye kusema maneno haya, kisha akafa katika usiku wake huo atakuwa amekufa juu ya umbile la kiisilam**”. Ameipokea Bukhari na Muslim kutoka kwa Baraa bin Aazib رضي الله عنه amesema, “alikuwa mtume ﷺ anapoliendea tandiko lake analala kwa ubavu wake wa kulia kisha anasema maneno haya ...”

**«بِاسْمِكَ رَبِّ وَضَعْتُ جَنْبِي وَبِكَ أَرْفَعُهُ إِنْ أَمْسَكْتَ نَفْسِي فَارْحَمْهَا وَإِنْ أَرْسَلْتَهَا فَاحْفَظْهَا بِمَا تَحْفَظُ بِهِ عِبَادَكَ الصَّالِحِينَ»**

5- «Kwa jina lako ewe mola wangu nimeweka mbavu zangu na kwako wewe naziinuwa, ikiwa kama utaizuia nafsi yangu basi irehemu na ikiwa kama utaiachia basi ihifadhi kwa kile unacho hifadhi kwacho waja wako wema». Ameipokea Bukhari na Muslim kutoka Abuu Huraira رضي الله عنه .

**«اللَّهَ أكبر (أَرْبَعًا وَثَلَاثِينَ) والحمد لله (ثَلَاثًا وَثَلَاثِينَ) وسبحان الله (ثَلَاثًا وَثَلَاثِينَ)**

6- Allahu Akbar(mara thelathini na nne) na Al-hamdu Lillahi(mara thelathini na tatu) na Subhana Llah (mara thelathini na tatu) “**hakika kufanya hivyo ni bora kuliko kuwa na mtumishi**”. Ameipokea Bukhari [2881] na Muslim kutoka kwa Ally رضي الله عنه . kutoka kwa mtume ﷺ akaitaja hadithi hii …..

**«اللَّهُمَّ رَبَّ السَّمَوَاتِ وَرَبَّ الأَرْضِ وَرَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ رَبَّنَا وَرَبَ كُلِّ شيء فَالِقَ الْحَبِّ وَالنَّوَى وَمُنْزِلَ التَّوْرَاةِ وَالإِنْجِيلِ وَالْفُرْقَانِ أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ كُلِّ شيء أَنْتَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهِ اللَّهُمَّ أَنْتَ الأَوَّلُ**

**فَلَيْسَ قَبْلَكَ شيء وَأَنْتَ الآخِرُ فَلَيسَ بَعْدَكَ شَيْءٌ وَأَنْتَ الظَّاهِرُ فَلَيسَ فَوْقَكَ شَيْءٌ وَأَنْتَ الْبَاطِنُ فَلَيْسَ دُونَكَ شَيْءٌ اقْضِ عَنَّا الدَّيْنَ وَأَغْنِنَا مِنَ الْفَقْرِ»**

7- «Ewe Allah mola wa mbingu na mola wa ardhi na mola wa arshi, mola wetu na mola wa kila kitu, mpasuwaji wa mbegu na kokwa na mteremshaji wa Taurati na Injili na Furqan(Qur'an), najikinga kwako kutokana na shari ya kila kitu, wewe ni mwenye kukishika utosi wake, ewe Allah wewe ni wa mwanzo hakuna kabla yako chochote na wewe ni wa mwisho hakuna baada yako chochote na wewe ni wa dhahiri hakuna juu yako chochote na wewe umefichikana hakuna chini yako chochote, tulipie sisi madeni na tutajirishe kutokana na ufakiri» kutoka kwa Abuu Huraira رضي الله عنه ameipokea Muslim [2713].

**«الحمد لله الذي أطعمنا وسقانا وكفانا وآوانا فكم ممن لا كافي له ولا مؤوي»**

8- «Sifa njema ni za Allah ambaye ametulisha na akatunywesha na akatutosheleza na akatupa makazi, ni wangapi ambao hawana wa kuwatosheleza wala hawana makazi». Ameipokea Muslim[2715] kutoka kwa Anas رضي الله عنه hakika ya mtume ﷺ alikuwa pindi anapo lielekea tandiko lake anasema, ….. mpaka mwisho.

**«اللهمَّ خَلَقْتَ نَفْسِي وَأَنْتَ تَوَفَّاهَا لَكَ مَمَاتُهَا وَمَحْيَاهَا إِنْ أَحْيَيْتَهَا فَاحْفَظْهَا وَإِنْ أَمَتَّهَا فَاغْفِرْ لَهَا اللهمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَافِيَةَ»**

9- «Ewe Allah umeiumba nafsi yangu na wewe unaifisha, ni kwako wewe kufa kwake na kuwa hai kwake, ikiwa kama utaipa uhai basi ihifadhi na ikiwa kama utaifisha basi isamehe, ewe Allah hakika mimi nakuomba afya». Ameipokea Muslim [4887] kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنه kutoka kwa mtume ﷺ.

**«اللهمَّ قِنِي عَذَابَكَ يَوْمَ تَبْعَثُ عِبَادَكَ»**( ثَلَاثَ مِرَارٍ).

10- «Ewe Allah nikinge mimi na adhabu yako siku utakapo wafufua waja wako». (mara tatu) kutoka kwa Hafswa رضي الله عنها mke wa mtume ﷺ "hakika ya mtume ﷺ alikuwa pindi anapotaka kulala, anaweka mkono wake wa kulia chini ya shavu lake, kisha anasema dua hii ....". Ameipokea Abuu Daud [4388] na hadithi hii iko katika Swahihi Musnad.

« اللهمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِوَجْهِكَ الْكَرِيمِ وَكَلِمَاتِكَ التَّامَّةِ مِنْ شَرِّ مَا أَنْتَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهِ اللهمَّ أَنْتَ تَكْشِفُ الْمَغْرَمَ وَالْمَأْثَمَ اللهمَّ لَا يُهْزَمُ جُنْدُكَ وَلَا يُخْلَفُ وَعْدُكَ وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ سُبْحَانَكَ وَبِحَمْدِكَ».

11- «Ewe Allah hakika mimi najikinga kwa uso wako mkarimu na maneno yako yaliyo kamilika kutokana na shari ya kile ambacho wewe ni mwenye kukishikilia utosi wake, ewe Allah wewe unaondoa madeni na madhambi, ewe Allah halishindwi jeshi lako na wala haikhalifiwi ahadi yako na hanufaishi mwenye utukufu, kwako wewe ndio unatoka utukufu, utakasifu ni wako na kuhimidiwa ni kwako». kutoka kwa Ally ﵁ kutoka kwa mtume ﷺ ‘‘kwamba yeye alikuwa akisema dua hii wakati wa kulala kwake’’. Ameipokea Abuu Daud[439] na hadithi hii iko katika Swahihi Musnad.

«الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي كَفَانِي وَآوَانِي وَأَطْعَمَنِي وَسَقَانِي وَالَّذِي مَنَّ عَلَيَّ فَأَفْضَلَ وَالَّذِي أَعْطَانِي فَأَجْزَلَ الْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى كُلِّ حَالٍ اللهمَّ رَبَّ كُلِّ شَيْءٍ وَمَلِيكَهُ وَإِلَهَ كُلِّ شَيْءٍ أَعُوذُ بِكَ مِنْ النَّارِ»

12- «Sifa njema ni za Allah ambaye amenitosheleza mimi na akanipa makazi na akanilisha na akaninywesha na ambaye ameneemesha juu yangu na kazidisha fadhila zake na ambaye amenipa mimi akakithirisha, sifa njema zinamstahiki Allah juu ya kila hali, ewe Allah mola wa kila kitu na mmiliki wake na mwabudiwa wa kila kitu, najikinga kwako kutokana na moto». kutoka kwa Ibn Umar ﵁ hakika ya mtume ﷺ alikuwa akisema wakati wa kulala kwake ….’’ mpaka mwisho. Ameipokea Abuu Daud [4399] na hadithi hii iko katika Swahihi Musnad.

# UTANGULIZI WA TAJWIIDI.

135 NI NGAPI HUKUMU ZA NUUN YENYE SAKNA NA TANWIIN?

JIBU: Ni nne;

Idh-hari; (kudhihirisha) na herufi zake ni,

( أ هـ ع ح غ خ ).

Id-gham; (kuingiza herufi kwenye herufi nyingine) na herufi zake zimekusanywa kwenye tamko hili,

(يرملون).

Iq-lab; (kuigeuza kuwa miim) na herufi yake ni,

(ب)

Ikh-faau; (kuificha) na herufi zake ni herufi zilizo bakia, nazo ni,

(ت ث ج د ذ ز س ش ص ض ط ظ ف ق ك)

136 NI IPI HUKUMU YA NUUN NA MIIM ZENYE SHADDA?

JIBU: hukumu yake ni kunung`unika kwa makadirio ya haraka mbili, mfano

النّاس . عمّ.

137 NI ZIPI HUKUMU ZA MIIM YENYE SAKNA?

JIBU: ina hukumu tatu, nazo ni Id-ghamu, Ikh-fau na Idh-hari.

Miim ikikutana pamoja na miim, huitwa id-gham mutamathileini (kuingiza herufi kwenye herufi mfano wake) mfano,

أطعمهم من جوع.

Miim ikikutana pamoja na bau, huitwa ikh-fau shafawiya, mfano

ترميهم بحجارة

Idh-hari shafawiy nayo inakuwa pamoja na herufi zote zilizo bakia.

138 NI ZIPI HERUFI ZA MADDA?

JIBU: herufi zake ni tatu, nazo ni alifu sakna ambayo ina fat-ha herufi iliyo kabla yake, mfano

(المهاد).

Na wau yenye sakna ambayo ina dhwa-mma herufi iliyo kabla yake. mfano

{يؤمنون}.

Yaa yenye sakna ambayo ina kasra herufi iliyo kabla yake, mfano

{رب العالمين}.

139 NI VIPI VIGAWANYO VYA MADDA?

JIBU: madda ambayo imesababishwa na hamza, nayo ni aina mbili;

Jaizil munfaswil; nayo ni ije herufi ya madda katika neno, na hamza katika neno jingine, mfano

{ إنا أرسلنا}

Wajibul mut-taswil; nayo ni ije herufi ya madda na hamza katika neno moja, mfano

{جآء}.

Madda ambayo sababu yake ni sukun nayo ni;

Maddu al-aridhwi li-ssukun(mada ambayo nimetokea kwa sababu ya sukuni) mfano

{المسلمين}

Maddul iwadhu, nayo ni kuzibadilisha fat'ha mbili kuwa alifu, mfano

{ثجاجًا}

Maddu laazim Alkilmiy al-muthaqal, nayo ni ije baada ya herufi ya madda herufi yenye shada, mfano

{الحاقّة}

Maddu laazim Akilimy al-mukhaffaf, nayo ni ije baada ya herufi ya madda herufi ambayo haina shada, mfano

**{آلْآن}**

140 NI IPI LAMU SHAMSIYYA NA LAMU QAMARIYYA?

JIBU: lamu shamsiyya ni ile ambayo inaandikwa lakini haitamkwi, nayo ni ile ambayo inafatwa na herufi hizi, nazo ni zilizo mwanzoni mwa kila neno katika ubeti huu,

**(طِبْ ثُمَّ صِلْ رُحْمًا تَفُزْ ضِفْ ذَا نِعَمْ دَعْ سُوءَ ظَنٍّ زُرْ شَرِيفًا لِلْكَرَمْ)**

Na lamul qamariyya nayo ni ile ambayo inaandikwa na inatamkwa, nayo ni,

(**ابغ حجك وخف عقيمه**).

# UTANGULIZI WA NAHAU.

141 KALAMU(MANENO) NI NINI?

JIBU: ni lafdhi iliyoundwa pamoja na nyingine, yenye faida, iliyowekwa kwa muweko wa kiarabu.

NI VIPI VIGAWANYO VYA KALAMU(MANENO)?

JIBU: vigawanyo vyake ni vitatu: jina, kitendo na herufi iliyo kuja kwa maana.

142 NI YAPI MAJINA ?

JIBU: Ni Ismul Mufrad Al-munswarif(jina la mtu mmoja lenye kuswarifika) na lina rufaishwa kwa dhwamma na linanasibishwa kwa fat'ha na linajurishwa kwa kasra. Mfano,

**(جاء محمدٌ) و (رأيت محمداً) (ومررت بمحمدٍ).**

Jamuu Taksiir Al-munswarif, nayo ni ile ambayo inabadilika sura ya wingi wake juu ya umoja wake na inarufaishwa kwa dhwamma na inanasibishwa kwa fat'ha na inajurishwa kwa kasra. Mfano,

**(جاء الطلاب) و(شاهدت الطالب) و(مررت بالطلاب).**

Jamul Muannath Saalim(wingi wa wanawake ulio salimika) nayo ni ile ambayo kumezidishwa katika umoja wake alifu na tau, na inarufaishwa kwa dhwamma ina nasibishwa kwa kasra na inajurishwa kwa kasra. mfano,

**(جاء المؤمناتُ) و(رأيت المؤمناتِ) و(مررت بالمؤمناتِ).**

Al-muthanna, nayo ni ile ambayo imezidi katika umoja wake alifu na nuun katika hali ya raf'u na inazidi yau na nuun katika hali ya nasb na jarri. Mfano,

**(صلى المسلمون) (وأكرمت المسلمين) و(مررت بالمسلمين).**

Jamuu mudhakkar saalim(wingi wa wanaume ulio salimika) nayo ni ile ambayo imezidi katika umoja wake wawu na nuun katika hali ya raf'u na inazidi yau na nuni wakati wa nasb na jarri. Mfano,

**(صلى المسلمون) (وأكرمت المسلمين) و(مررت بالمسلمين).**

As-maaul khamsa(majina matano) nayo ni,

**أبوك وأخوك وحموكِ وفوك وذو مال**

Yanarufaishwa kwa wawu na yananasibishwa kwa alifu na yanajurishwa kwa yau mfano,

**(حضر أبوك) و(رأيت أباك) و(مررت بأبيك).**

143 NI ZIPI DHWAMIRI?

JIBU: ni dhwamiri ya mzungumzaji iliyounganika, mfano

**ضربتُ وضربنا.**

Na dhwamiri ya mzungumzaji iliyotenganishwa, mfano

**أنا ونحن.**

Na dhwamiri ya mukhatwabul munfaswil(mwenye kuzungumzishwa iliyotenganishwa ) , mfano

**أنت وأنتِ أنتما أنتم أنتن.**

na dhwamiril ghaaibul munfaswil(ambaye hayupo iliyotenganishwa) , mfano

**هو وهي هما هم هن.**

Na dhwamiri ya mukhatwabul muttaswil(mwenye kuzungumzishwa iliyounganika) , mfano

**ضربتَ ضربتِ ضربتما ضربتم ضربتن.**

Na dhwamiril ghaaibul muttaswil(ambaye hayupo aliyounganika ) , mfano

**: ضرب ضربَت ضربا ضربوا ضربن.**

144 VITENDO VINAGAWANYIKA SEHEMU NGAPI?

JIBU:1-al-maadhwi (kitendo cha wakati uliopita). mfano,

دخلَ.

2- al-mudhwaariu(kitendo cha wakati uliopo). mfano,

، يدخلُ

3-al-amru(kitendo cha kuamrisha). Mfano,

ادخلْ.

# UTANGULIZI WA MUSTWALAH KATIKA HADITHI.

145 NI IPI HADITHI SAHIHI?

JIBU: ni ile ambayo imeunganika sanadi yake, kwa nukuu ya mtu muadilifu, mwenye kudhibiti, mpaka mwisho wa sanadi, na haikuwa ni shadha wala haina dosari.

146 NI IPI HADITHI HASAN ?

JIBU: ni ile ambayo kumepunguwa udhibiti kwa wapokezi wake, au akawa ni dhaifu, udhaifu ambao unaweza kutiliwa nguvu na hadith nyingine, ikawa ni hasan.

147 NI IPI HADITHI DHAIFU?

JIBU: ni ile ambayo kumepungua ndani yake sharti miongomi mwa masharti ya hadithi sahihi na hasan.

148 NI IPI HADITHI MAR'FUU?

JIBU: ni kauli ya mtume ﷺ na kitendo chake na kukiri kwake juu ya kitu chochote.

- NI IPI HADITHI MAU'QUF?

JIBU: ni kauli ya swahaba na kitendo chake.

- NI IPI HADITHI MAQ'TUU?

JIBU: ni kauli ya taabiiy(ni yule aliyekuja baada ya maswahaba) na kitendo chake.

- NI IPI HADITHI MUN’QATWII?

JIBU: ni ile ambayo ameanguka katika sanadi yake, mpokezi mmoja au zaidi.

149 NI IPI HADITHI MUU’DHWAL?

JIBU: ni ile ambayo wameanguka katika sanadi yake, wapokezi wawili na zaidi kwa kufuatana.

150 NI IPI HADITHI MUR’SAL?

JIBU: ni ile ambayo kaiegemeza taabiiy kwa mtume ﷺ moja kwa moja, pasina ya kumtaja swahaba.

151 NI IPI HADITHI MU’ALLAQ?

JIBU: ni ile ambayo pameangushwa mwanzoni mwa sanadi yake mpokezi mmoja au zaidi.

152 NI IPI HADITHI MAU’DHUU?

JIBU: ni ile ambayo imesingiziwa kwa mtume ﷺ.

153 TAJA MIONGONI MWA MUTUUNI MUHIMU?

JIBU: Laamiyya ya Sheikhul Islaam Ibn Taymiyyah,

## LAAMIYYAH

يا سـائلي عـن مذهبـي وعقـيـدتـي رزق الـهدى من للـهداية يسأل

Ewe mwenye kuniuliza mimi kuhusu madhehebu yangu na akida yangu, ameruzukiwa uongofu mwenye kuuliza kwa ajili ya kuongoka.

اسمـع كـلام محـقـق فـي قولـــه لا ينـثـنـي عنـه ولا يـتـبـدل

Sikiliza maneno ya mwenye uhakika katika kauli yake, harejei kuachanana nayo na wala habadiliki.

حب الصحابة كلهم لي مذهب ومودة القـربى بها أتوسـل

Kuwapenda maswahaba wote kwangu mimi ndio madhehebu yangu, na kuwapenda ndugu za Mtume ﷺ kwa mapenzi hayo nafanya tawassul.

ولـكلهـم قـدر وفضـل ساطـع لكنما الصديق منـهم أفضـل

Na anacho kila mmoja wao cheo na fadhila za juu, lakini si vinginevyo Swiddiiq katika wao ni mbora zaidi.

وأقول في القرآن ما جاءت به آيـاتـه فـهـو الكريـم المنـزل

Na ninasema katika Qur’an kile ambacho imekuja nacho, ni aya zake Allah nayo hiyo Qur,an ni tukufu yenye kuteremshwa.

وأقــول قــال الله جــل جــلالـــه والمصطفى الهادي ولا أتأول

Na ninasema amesema Allah umetukuka utukufu wake, na Mustwafaa(mtume) mwenye kuongoza wala sifanyi taawili.

وجميع آيـات الصفـات أمرُّهـا حقـاً كما نقـل الطـراز الأول

Na aya zote za sifa nazipitisha, kwa uhakika kabisa kama walivyo nukuu kundi la mwanzo.

وأرد عـهـدتــهـا إلـى نـقّـالـهـا وأصونـهـا عن كل ما يُتخـيـل

Na ninarudisha dhamana yake kwa wanukuzi wake, na ninazilinda kutokana na kila chenye kudhaniwa kibaya.

قبحاً لمن نبـذ القـرآن وراءه وإذا استدل يقول قال الأخطل

Ni ubaya ulioje kwa mwenye kuitupa Qur'an nyuma yake, na anapotoa dalili anasema amesema Akh-twalu(mkiristo).

والمؤمنون يرون حقاً ربهـم وإلى السماء بغير كيف ينزل

Na waumini watamuona kwa uhakika kabisa mola wao, na kuielekea mbingu ya dunia bila namna anashuka(Allah).

وأقر بالميزان والحوض الذي أرجـو بأنــي مـنــه ريـاً أنــهـل

Na ninakiri mizani na hodhi ambalo, natarajia kuwa mimi kutokana na hodhi hilo kiu nitakata.

وكذا الصـراط يمد فوق جهنم فـمـوحـد نــاج وآخــر مـهـمـل

Na hivyohivyo swiratwi(njia) itakunjuliwa juu ya jahannam, basi mwenye kumpwekesha Allah ni mwenye kuokoka na mwingine (asiye mpwekesha Allah) ni mwenye kupuuzwa.

والنـار يصلـها الشقي بحـكمـة وكذا التقي إلى الجنان سيدخل

Na moto atauingia muovu kwa hekima yake Allah, na hivyohivyo mwenye kumcha Allah katika mabustani ataingia.

ولكل حي عـاقـل فـي قـبـره عـمـل يـقــارنــه هنــاك ويسـأل

Na analo kila aliye hai mwenye akili katika kaburi lake, tendo ambalo litasuhubiana naye huko na ataulizwa.

هذا اعتقاد الشافـعي ومـالـك وأبي حـنـيـفـة ثـم أحمـد يـنـقـل

Hii ni itikadi ya Shaafiiy na Maalik, na Abuu Haniifa kisha Ahmad hunukuliwa.

فـإن اتبـعـت سبيلـهـم فموفـق وإن ابتـدعت فما عليـك معول

Ikiwa utafuata mwenendo wao basi utakuwa ni mwenye kuafikishwa, na ikiwa utazusha basi huna wewe mahali pakuegemea.

# HAAIYYA YA IBN ABII DAUD

**تمسك بحبلِ الله واتبعِ الهُدى ولا تكُ بدعيا لعلك تُفلحُ**

Shikamana na kamba ya Allah na fuata uongofu, na wala usiwe mtu wa bidaa(mzushi) bila shaka hutofaulu.

**ودنْ بكتابِ الله والسننِ التي أتت عنْ رسول الله تنجو وتربحُ**

Na fanya dini kwa kitabu cha Allah na sunna ambazo, zimekuja kutoka kwa mtume ﷺ utaokoka na utapata faida.

**وقل غيرُ مخلوقٍ كلام مليكنا بذلك دان الأتقياء وأفصحوا**

Na sema si kiumbe maneno(Qur'an) ya mfalme wetu, kwa itikadi hiyo walifanya dini wema na wakaliweka wazi.

**ولا تكُ في القرآن بالوقف قائلاً كما قال أتْباعٌ لجمٍ وأسجحُوا**

Na wala usiwe katika Qur'an ni mwenye kusema kwa kusita, kama walivyo sema wafuasi wa Jahami na Nyoyo zao zikaridhia hii itikadi mbaya.

**ولا تقل القرآن حلْقٌ قرأْتُهُ فإن كلام اللهِ باللفظ يُوضحُ**

Na wala usiseme kuwa Qur'an ni kiumbe nimekisoma, kwa hakika maneno ya Allah kwa lafdhi yanawekwa wazi.

**وقل يتجلى الله للخلقِ جهرةً كما البدر لا يخفى وربك أوضحُ**

Na sema atajidhihirisha Allah kwa viumbe kwa uwazi, kama mwezi mpevu haufichikani na mola wako yuko wazi mno.

**وليس بمولودٍ وليس بوالدٍ وليس له شِبْهٌ تعالى المُسبحُ**

Na si mzaliwa na wala si mzazi, na hana mfano yeye ametukuka mwenye kutakaswa.

**وقد يُنكِر الجهمي هذا وعندنا بمصداقِ ما قلنا حديثٌ مصرحُ**

Na kwa hakika anapinga hili Jahami na sisi tunayo, kwa kusadikisha yale tuliyo yasema hadithi iliyo wazi.

رواه جريرٌ عن مقالِ مُحمدٍ فقلْ مِثل ما قد قال في ذاك تنْجحُ
Ameipokea Jariir kutoka katika maneno ya Muhammad, basi sema mfano wa kile alicho kisema katika hilo utafaulu.

وقد ينكرُ الجهمي أيضاً يمينهُ وكِلتا يديه بالفواضلِ تنْفحُ
Na kwa hakika anapinga Jahami pia mkono wake wa kulia, na mikono yake yote miwili kwa kipao inatoa.

وقل ينزلُ الجبارُ في كلِّ ليلةٍ بلا كيفَ جلَّ الواحدُ المُتمَدحُ
Na sema anateremka Al-Jabbaar katika kila usiku, bila ya namna ametukuka Mmoja mwenye kusifiwa.

إلى طبقِ الدنيا يمُنُّ بفضلهِ فتفرجُ أبواب السماءِ وتُفتحُ
Mpaka katika tabaka ya dunia anatoa kwa fadhila zake, na inaachwa wazi milango ya mbingu na Inafunguliwa.

يقولُ أَلا مُستغفرٌ يَلقَ غافراً ومُستمنحٌ خيراً ورِزْقاً فُيمنحُ
Anasema hivi kuna mwenye kutaka msamaha akutane na mwenye kusamehe, na mwenye kutaka kheri Na rizki ili apewe.

روى ذاك قومٌ لا يردُّ حديثُهم ألا خابَ قومٌ كذبوهم وقُبِّحوا
Wamelipokea hilo watu ambao hazirudishwi hadithi zao, tambua, ni wenye kupata hasara watu ambao Wamewakadhibisha na wamelaaniwa.

وقل: إنَّ خير النَّاسِ بعد محمَّدٍ وزيراهُ قدماً ثم عثمانُ الأرجَحُ
Na sema hakika mbora wa watu baada ya Muhammad, ni mawaziri wake toka mwazo kisha Uthmaan Kwa kauli yenye nguvu.

ورابعهُمْ خيرُ البريَّة بعدهُم عليٌّ حليفُ الخيرِ بالخيرِ مُنْجِحُ
Na wa nne wao ni mbora wa viumbe baada yao, Ally mwenye kulazimiana na kheri kwa kheri ni mwenye Kufaulu.

وإنهم للرهط لا ريب فيهم على نُجبِ الفردوسِ بالنّور تَسرحُ
Na hakika wao ni kundi ambalo hakuna shaka kwao wao, juu ya mito ya firdaus kwa nuru roho zao ni zenye Kwenda na kurudi.

سعيدٌ وسعدٌ وابن عوفٍ وطلحة وعـامـرُ فـهـرٍ والـزبـيـرُ المـمـدَّح

Said na Saad na Ibn Auf na Twalha, na Aamir Fihrin na Zubeir mwenye kusifiwa.

وقل خير قولٍ في الصحابة كلِّهم ولا تـك طـعَّـانـاً تعـيــبُ وتـجـرحُ

Na sema kauli nzuri kwa Maswahaba wote, na wala usiwe mwingi wa kuwatukana unawatia aibu na unawajeruhi.

فقد نطقَ الوحيُ المبين بفضلِهم وفـي الفتـح آيٌ للصَّحـابـةِ تمـدحُ

Na kwa hakika umetamka wahyi ulio wazi juu ya fadhila zao, na katika Suratul Fathi kuna aya ambazo zinawasifu maswahaba.

وبـالقـدرِ الـمـقـدورِ أيـقِـن فإنَّــه دعـامـةُ عقـدِ الدِّيـن والدِّيـنُ أفيـحُ

Na kwa kadari ya makadirio kuwa na yakini hakika, hiyo kadari ni nguzo ya dini na dini ni pana.

ولا تُنكِرَنْ جهلاً نكيـراً ومُـنـكـراً ولا الحوْضَ والمِيزانَ إنك تُنصحُ

Na wala usipinge kwa ujinga Nakiri na Munkar, na wala hodhi na mizani hakika wewe unanasihiwa.

وقُلْ يُخـرجُ اللهُ الْعـظـيـمُ بِفَضْـلِهِ من النـار أجسادا من الفحم تطرح

Na sema anatoa Allah mkubwa kwa fadhila zake, motoni miili ambayo inatokana na mkaa kisha Itatupwa.

عَلى النهرِ في الفِرْدوسِ تَحْيَا بِمَائِهِ كَحِبِّ حَمِيـلِ السَّيْلِ إذْ جَـاءَ يَطْفَـحُ

Juu ya mto katika firdaus itapata uhai kwa maji yake, kama vile mbegu iliyobebwa na mafuriko pindi Yalipo kuja yanaruka.

وإن رَسُــولَ اللهِ لـلـخَـلْــقِ شَـافِــعٌ وقُلْ في عَذابِ القَبْرِ حَقّ مُوَضحُ

Na kwa hakika mtume wa Allah kwa viumbe ni mwenye kuwaombea, na sema katika adhabu ya kaburi Ni haki iliyo wazi.

ولاَ تُكْفِرنْ أَهلَ الصلاةِ وإنْ عَصَوْا فَكُلـهُمُ يَعْصـِي وذُو العَرشِ يَصفَحُ

Na wala usiwakufurishe watu wa swala hata kama wakiasi, kwani kila mwanadamu anafanya maasi Na mwenye arshi anasamehe.

**وَلَا تَعتَقِدْ رأيَ الْخَوَارجِ إِنهُ مقَالٌ لَمنْ يَهواهُ يُردي ويَفْضَحُ**

Na wala usiitakidi rai ya Khawaarij kwani hayo, ni maneno ambayo mwenye kuyaitakidi yanamuangamiza na Yanamfedhehesha.

**ولا تكُ مُرْجيًّا لَعُوبا بدينهِ ألاَ إِنمَا المُرْجِي بِالدينِ يَمْزحُ**

Na wala usiwe Murjia mwenye kucheza na dini yake, fahamuni hakika si vinginevyo Murjia wanaifanyia mzaha dini.

**وقلْ: إنمَا الإِيمانُ: قولٌ ونِيةٌ وفعلٌ عَلَى قولِ النبِي مُصَرحُ**

Na sema hakika si vinginevyo imani ni: kauli na nia, na kitendo juu ya kauli ya Nabii iliyo wazi.

**ويَنْقُصُ طوراً بالمَعَاصِي وتَارةً بِطَاعَتِهِ يَمْنَي وفي الوَزْنِ يَرْجَحُ**

Na inapungua wakati mwingine kwa maasi na wakati mwingine, kwa kumtii Allah inazidi na katika mizani Inakuwa nzito.

**ودعْ عَنْكَ آراءَ الرجالِ وقَوْلَهُمْ فقولُ رسولِ اللهِ أزكَى وأَشْرحُ**

Na acha wewe rai za watu na kauli zao, kwani kauli ya mtume wa Allah ni bora na ni kunjufu mno.

**ولا تَكُ مِن قوْمٍ تلهوْا بدينِهِمْ فَتَطْعَنَ في أهلِ الحَديثِ وتقدحُ**

Na wala usiwe miongoni mwa watu ambao wamechezea dini yao, ukawa unawasema vibaya watu wa hadithi na unawatia dosari.

**إذاما اعتقدت الدَّهْر ياصاح هَذِه فَأَنت على خير تبيت وتصبح**

Pindi utakapoitakidi hivi milele ewe rafiki, hakika utakuwa katika kheri nyakati za jioni na asubuhi.

# BAIQUUNIYYA

**أبدأُ بالحمدِ مُصَلِّياً عَلَى    مُحَمَّدٍ خَيْرِ نبيْ أُرسلا**

Ninaaza kwa kuhimidi hali ya kumswalia, Muhammad nabii mbora aliyetumwa.

**وذِي من أقْسَامِ الحَدِيثِ عِدَّهْ    وَكُلٌّ واحد أتى وحدَّه**

Na hivi ni miongoni mwa vigawanyo vingi vya hadithi, na kila kimoja kimekuja na maana yake.

**أوَّلُها الصَّحِيحُ وَهْوَ مَا اتَّصل    إسْنَادُهُ وَلَمْ يَشُذَّ أَوْ يُعَلْ**

Kigawanyo cha kwanza ni SAHIHI nayo ni ile ambayo imeunganika, isnadi yake na haikuwa shadha wala haikuwa na dosari.

**يَرْوِيهِ عَدْلٌ ضَابِطٌ عَنْ مِثْلِه    مُعْتَمَدٌ فِي ضَبْطِهِ وَنَقْلِه**

Anaipokea mwadilifu mwenye kudhibiti kutoka kwa mfano wake, mwenye kutegemewa katika udhibiti wake na unukuzi wake.

**والَحسَنُ المعروفُ طُرْقاً وَغَدَتْ    رِجَالُهُ لاَ كالصّحيحِ اشْتَهَرَتْ**

Na HASAN ni ile yenye kujulikana njia zake na wakawa, wapokezi wake si kama wapokezi wa hadithi Sahihi imekuwa mashuhuri.

**وكُلُّ مَا عَنْ رُتْبَةِ الحسن قصر    فهو الضعيف وَهْوَ أَقْسَاماً كُثُر**

Na kila ile ambayo imepunguwa kutoka katika daraja ya hadithi hasan, basi hiyo ni DHAIFU nayo ni vigawanyo vingi.

**وَمَا أُضيفَ للنَّبِي المَرْفُوعُ    وَمَا لِتَابِعٍ هو المقطوع**

Na ile hadithi iliyoegemezwa kwa Mtume ni MAR’FUU na ile iliyoegemezwa kwa Taabiiy ni MAQ’TUU.

**والُمسنَدُ الُمتَّصِلُ الإسنادِ مِنْ    رَاوِيهِ حَتَّى المُصْطَفَى وَلَمْ يَبِنْ**

Na hadithi MUSNAD ni ile ambayo imeunganika sanadi yake kuanzia, kwa mpokezi wake mpaka kwa Mtume ﷺ na haikuachana.

وَمَـا بِسَمْـعِ كُـلِّ رَاوٍ يَـتَّصِـلْ إسْنَـادُهُ لِلْمُصْطَفَـى فَالْمُتَّصِلْ

Na hadithi ambayo imeunganika sanadi yake kwa kusikia kila mpokezi kutoka kwa mpokezi mwingine Mpaka kwa mtume basi hiyo ni hadithi MUT-TASWIL.

مُسَلْسَلٌ قُلْ مَـا عَلَى وَصْفٍ أَتَـى مِـثْلُ أَمَـا وَاللهِ أنْبـأنِـي الْـفَـتَـى

MUSALSAL sema ni ile ambayo imekuja juu ya sifa fulani, mfano namuapia Allah, ameniambia mimi Kijana.

كـذَاكَ قَـدْ حَـدَّثَـنِـيـهِ قَـائـمـا أَوْ بَـعْـدَ أَنْ حَـدَّثَـنِـي تَـبَـسَّـمَـا

Hivyo hivyo kama kusema amenisimulia mimi hadithi hii hali ya kuwa amesimama, au baada ya Kunisimulia alitabasamu.

عَزِيـزُ مَـرْوِي اثْـنَـيْـنِ أوْ ثَـلاَثَـهْ مَشْهُورُ مَرْوِي فـوْقَ مَا ثَلاثَـهْ

Hadithi AZIZI ni ile ambayo imepokelewa na wawili au watatu, na hadithi MASHUHUR ni ile iliyopokelewa Na watu zaidi ya watatu.

مـعَنْعَنٌ كَـعَن سَـعِيـدٍ عَنْ كَـرَمْ وَمُـبْـهَـمٌ مَـا فِيـهِ رَاوٍ لَـمْ يُسَمْ

Hadithi MUAN’AN ni ile ambayo imepokelewa kwa kutumia lafdhi ya AN kama vile AN SAID(kutoka kwa Said) AN KARAM(kutoka kwa Karam) na hadithi MUB’HAM ni ile ambayo ndani yake kuna mpokezi ambae hajatajwa jina lake.

وَكُـلُّ مَـا قَـلَّـتْ رِجَـالُـهُ عَـلاَ وَضِـدُهُ ذاك الـذي قـد نَـزَلا

Na kila Isnadi ambayo wamepunguwa wapokezi wake inakuwa ni Isnadi iliyo juu, na kinyume chake hiyo ndiyo ambayo kwa hakika inakuwa imeshuka.

ومَـا أضَفْتَـهُ إِلَـى الأَصْحَـابِ مِـنْ قَوْلٍ وفعل فهو مَوْقُوفٌ زُكِـنْ

Na ile ambayo umeiegemeza kwa maswahaba miongoni mwa kauli au kitendo basi hiyo ni MAU’QUUF Imefahamika.

وَمُرْسـلٌ مِنْـهُ الصِّحَـابِيُّ سَـقَــطْ وَقُلْ غَرِيبٌ مَا رَوَى رَاوٍ فَقَـط

Na hadithi MURSAL ni ile ambayo ajatajwa ndani ya sanadi yake swahaba, na sema hadithi GHARIB Ni ile ambayo ameipokea mpokezi mmoja tu.

وَكُلُّ مَا لَمْ يَتَّصِلْ بحال          إسْنَادُهُ مُنْقَطِعُ الأوْصالِ

Na kila hadithi ambayo isnadi yake haijaunganika kwa hali yoyote, basi isnadi yake ni MUNQATWI (iliyokatika wapokezi wake).

والْمعْضَلُ الساقِط مِنه اثنانِ          وما أتى مُدلساً نَوعانِ

Na hadithi MU’UDHWAL ile ambayo wameanguka ndani ya sanadi yake wawili, na ile hadithi Ambayo imekuja hali ya kuwa ni MUDALLAS iko aina mbili.

الأَوَّلُ: الاسْقَاطُ لِلشَّيْخِ وَأَنْ          ينقلُ عَمَّنْ فَوْقَهُ بِعَنْ وَأَنْ

Ya mwanzo katika Mudallas ni mpokezi kumuangusha Shekhe wake na, akanukuu kwa aliye juu ya Shekhe wake kwa Kutumia lafdhi ya A’N na AN.

والثَّانِ: لاَ يُسْقِطُهُ لَكِنْ يَصِفْ          أَوْصَافَهُ بِمَا بِهِ لاَ ينعرف

Na aina ya pili hamuangushi Shekhe wake lakini anamsifu, kwa sifa ambazo hawezi kufahamika.

وما يخالف ثِقَةٌ بِهِ المَلأ          فالشاذُّ والَمقْلُوبُ قِسْمَانِ تَلا

Na ile hadithi ambayo anakhalifu ndani yake mtu muadilifu watu walio bora kuliko yeye, basi hiyo ni SHADHA Na hadithi MAQ’LUUB ni vigawanyo viwili vyenye kufuatana.

إبْدَالُ رَاوٍ مَا بِرَاوٍ قِسْمُ          وَقَلْبُ إسْنَادٍ لمَتْنٍ قِسْمُ

Kumbadilisha mpokezi kwa mpokezi mwingine ni kigawanyo, na kubadilisha sanadi kwa matni nyingine hiki ni kigawanyo kingine.

والفَردُ مَا قَيَّدْتَهُ بِثِقَةِ          أَوْ جَمْعٍ أوْ قَصْرٍ عَلَى روايةِ

Na FARDU ni ile ambayo umeifungamanisha kwa muadilifu, au kundi kutoka katika mji fulani au kusema hajapokea fulani isipokuwa kwa fulani tu.

ومَا بعِلَّةٍ غُمُوضٍ أَوْ خَفَا          مُعَلَّلٌ عِنْدَهُمُ قَدْ عُرِفَا

Na hadithi ambayo ina dosari iliyofichikana sana au kidogo, basi hadithi hiyo ni MUALLAL kwao wao(watu wa hadithi) kwa hakika imefahamika.

وذُو اخْـتِـلافِ سَـنَـدٍ أَوْ مَـتْـنِ مُضْطَـرِبٌ عِنْدَ أُهَـيْلِ الْفَنِّ

Na hadithi ambayo ina ikhtilafu nyingi za kisanadi au kimatni, ni MUDH'TWARIB kwa watu wa fani ya Mustwalah.

والُمـدْرَجَـاتُ فِي الحديـثِ مَا أَتَـت مِـنْ بَعْض أَلْفَاظِ الرُّوَاةِ اتَّصَلَتْ

Na MUD'RAJ katika hadithi ni zile ambazo zimekuja kutoka, katika baadhi ya lafdhi za wapokezi ambazo zimeunganikana na hadithi.

ومَـا رَوى كُـلُّ قَـرِيـنٍ عَنْ أَخِـهْ مُـدّبَّجٌ فَأَعْـرِفْـهُ حَـقًّـا وانْـتَـخِـهْ

Na ile iliyopokelewa na mtu wa rika moja kutoka kwa ndugu yake, ni MUDABBAJ basi ifahamu ukweli wa kuifahamu na jifakharishe.

مُـتَّـفِـقٌ لَـفْـظـاً وَخَـطـاً مُـتَّـفِـقْ وضِـدُّهُ فِـيـمَـا ذَكَـرْنَـا الـمُـفْـتَـرِقْ

Na ile ambayo yamewafikiana majina ya wapokezi kilafdhi na kimaandishi ni MUT'TAFIQ, na kinyume cha yale tuliyoyataja ni MUF'TARIQ.

مُـؤْتَـلِـفٌ مُـتَّـفِـقُ الـخَـطِّ فَـقَـطْ وَضِـدُّهُ مُـخْـتَـلِـفُ فَـاخْـشَ الْغَلَطْ

MU'UTALIF ni ile ambayo yamewafikiana majina ya wapokezi kimaandishi tu, na kinyume chake ni MUKH'TALIF basi ogopa kukosea(kujichanganya).

وَالمُـنْـكَـرُ الْفَـرْدُ بِـهِ رَاوٍ غَـدَا تَـعْـدِيـلُـهُ لاَ يَـحْـمِـلُ الـتَّـفَـرُّدَا

Na MUNKAR ni ile ambayo amepwekeka nayo mpokezi mmoja, ambaye kumekuwa kumuadilisha kwake Hakukubali kupwekeka nayo.

مَـتْـرُوكُـهُ مَـا وَاحِـدٌ بِـهِ انْـفَـرَدْ وَأَجْـمَـعُـوا لِـضَـعْـفِـهِ فَـهْـوَ كَـرَدْ

Hadithi MAT'RUUK ni ile ambayo kapwekeka nayo mtu mmoja, na wamekubaliana wanachuoni kwa udhaifu wake basi hadithi hii ni kama yenye kurudishwa.

وَالـكَذِبُ المُـخْـتَـلَـقُ المَـصْـنُـوعُ عَـلَى الـنَّـبِـي فَـذلِـكَ المـوْضـوعُ

Na uongo wenye kuzushwa wenye kutengenezwa, juu ya Nabiiy ﷺ basi hiyo ndiyo hadithi MAUDHWUU.

وَقَدْ أَتَـتْ كَالـجَـوْهَـرِ المَكْنُـونِ سَمَّيْتُهَا مَنْـظُـومَـةَ الـبَـيْـقُـونـي

Na kwa hakika umekuja utenzi huu kama johari iliyohifadhiwa, nimeuita MANDHUUMATUL BAYQUUNIY.

فَـوْقَ الثَّـلاثـيَـن بـأَرْبَـعٍ أتَـت أقْسامُهَا تَمَّتْ بِـخَـيْرٍ خُتِمَـتْ

Imekuja na beti thelathini na nne, vigawanyo vyake vimekamilika na vimekhitimishwa kwa kheri.

# YALIYOMO.

UTANGULIZI........................................................................3
AQIIDA...........................................................................5
TWAHARA NA SWALA ........................................................31
ZAKA ............................................................................34
SWAUMU ........................................................................35
HIJJA.............................................................................37
FAIDA TOFAUTI TOFAUTI.....................................................39
UTANGULIZI WA TAJWIIDI....................................................65
UTANGULIZI WA NAHAU. .....................................................68
UTANGULIZI WA MUSTWALAH KATIKA HADITHI.......................71
LAAMIYAH.......................................................................73
HAIYYA YA IBN ABII DAUD ..................................................75
BAIQUNIYA......................................................................79
YALIYOMO.......................................................................84